# Nipashe
MWANGA WA JAMII

Jumapili Julai 25, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

JUMAPILI

ISSN 0856 • No. 0580652





UKURASA 15

## MO DEWJI AMWAHIDI
Rais Samia ajira 100,000, ufadhili wa mabilioni kwa Sekta ya Elimu



UKURASA 2

## WATUMIAJI
wa bangi nchini waongezeka

UKURASA 2

## RIPOTI MAALUM:
# Kufuru ya posho ATCL

Wafanyakazi walipana mabilioni kinyume cha sheria...

*Endelea UK. 4 & 5*




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Liberata Mulamula (katikati) na Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, wakiangalia sehemu ya shehena ya chanjo ya COVID-19, iliyowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, ikitokea nchini Marekani. **PICHA: ANTHONY SIAME**

## Mpango: 'Tumezimiss' busara za Mkapa CCM



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na mkewe Mama Mbonimpawe Mpango, wakiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, kijijini Lupaso, Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara jana, baada ya kuhudhuria misa ya kumbukizi ya mwaka mmoja tangu kifo chake. Habari Uk. 3. **PICHA: OMR**

## Mikoa 10 kipaumbele chanjo ya corona hii

UK. 2

**MICHEZO** SIKU YA HUKUMU IMEWADIA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Mikoa 10 kipaumbele chanjo corona hii

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imepokea msaada wa chanjo ya Corona kutoka Marekani na kueleza kuwa baada ya kujiridhisha kuwa ni salama utolewaji wake utafanyika nchi nzima lakini kwa kuanza na mikoa 10 ya kipaumbele.

Mikoa hiyo ya kipaumbele ni Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya, Arusha, Kigoma, Singida, Dodoma, Iringa na Mtwara.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere baada ya kupokea msaada wa dozi zaidi ya milioni moja za chanjo ya corona aina ya Johnson & Johnson.

Alisema msaada huo umetolewa na Marekani ikiwa sehemu ya ahadi ya nchi hiyo ya kutoa angalau dozi milioni 25 kwa Afrika kati ya dozi milioni 80 zilizoahidiwa kwa bara hilo.

Waziri huyo aliishukuru Marekani kwa mchango mkubwa wa kutoa chanjo kwenye mpango wa COVAX Facility ambao umewezesha Tanzania kuwa nchi mojawapo kupata dozi 1,058,400 zitakazosaidia kupambana na corona.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha angalau asilimia 60 ya Watanzania wanapata chanjo hata baada ya hizo kutumika.

"Chanjo hii itaanza baada ya watalaamu kujiridhisha, wataalamu wetu wanafanya taratibu za kujiridhisha kabla ya kuanza mchakato wa kuchanja. Ninawaomba wananchi wajitokeze pindi tukianza," alisema.

Dk. Gwajima alisema serikali itapokea chanjo ya aina nyingine katika wiki zijazo ili kuhakikisha watu wote wanapata huduma hiyo na kipaumbele kikiwa ni wahudumu wa afya, watu wazima kuanzia miaka 50 na wenye magonjwa sugu katika mikoa hiyo 10.

"Kama ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Rais John Magufuli, ilielekeza kuwa 'Wizara ya Afya ijiridhishe kabla ya kupokea chanjo hizo', wizara haitapokea chanjo hadi ijiridhishe," alisema.

Dk. Dorothy alisema kuwa kupitia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, wizara imetimiza wajibu wa kujiridhisha.

Alisema mara baada ya kujiridhisha, serikali itaanza kutoa chanjo hiyo katika vituo mbalimbali vya afya kwa mujibu wa miongozo iliyopo na kuwataka wahusika kuwajibika ili Watanzania waipate.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Abeli Makubi, alilishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na WHO kwa kufanikisha Tanzania kupata shehena ya dozi hiyo ya kwanza.

Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, alisema msaada wa chanjo utasaidia kuwalinda Watanzania dhidi ya corona na kupunguza vikwazo katika jitihada za kuujenga upya uchumi wa Tanzania.

Mwakilishi Mkazi wa UNICEF, Shalini Baliaguna, aliitaka jamii kujiepusha na uvumi unaotangazwa mitandao ya kijamii kuhusu corona na kutaka watu watafute taarifa sahihi vyanzo rasmi.

Mwakilishi Mkazi wa WHO, Dk. Tigast Mengistu, alisema Tanzania itakuwa imepiga hatua kubwa mbele kwa kuwachanja watu wake.

Alisema wapo tayari kusaidia Tanzania kuhakikisha chanjo inawafikia watu wote waliopo.

## Watumiaji bangi waongezeka

**Na Gwamaka Alipipi**

WATUMIAJI wa dawa za kulevya aina ya bangi nchini wameongezeka, huku uingizaji wa dawa kutoka nje ya nchi ukiwa umedhibitiwa kwa asilimia 95.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Ajira, Tixon Nzunda, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipotembea Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Nzunda alisema DCEA imejitahidi kwa asilimia kubwa katika kupambana na kudhibiti uingizaji na matumizi ya dawa za kulevya kutoka nje ya nchi, lakini bado kuna tatizo kubwa la matumizi na ulimaji wa bangi. Nzunda alisema: "DCEA tangu imeanzishwa, wamejitahidi kuimarisha mifumo ya kisera na kikanuni. Serikali tumekuwa tukiwapa ushirikiano mkubwa katika mapambano ya dawa za kulevya. 'Katika mafanikio hayo, wamefanikiwa kudhibiti asilimia 95 ya dawa za kulevya zitokazo nje ya nchi kuingia nchini."

Nzunda alisema licha ya mafanikio hayo, watumiaji wa dawa za kulevya aina ya bangi bado ni wengi na idadi inaongezeka kwa kasi, hivyo jitihada zinahitajika za kuanzisha vita dhidi ya kilimo cha bangi.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, alisema kuanzia mwaka 2013 hadi 2014 kabla ya kuanzishwa kwa DCEA, uingizaji wa dawa za kulevya aina ya heroin nchini ulikuwa ni wa asilimia 88, lakini baada ya mamlaka kuanzishwa mwaka 2015 na kuanza kazi mwaka 2017, kiwango cha uingizaji wa dawa za kulevya aina hizo kilishuka hadi asilimia tano.

"Tatizo la matumizi ya bangi bado lipo juu na linaongezeka, hadi sasa tumekamata milioni ya kilo za bangi, operesheni tunaziendesha kila siku lakini tatizo bado lipo kulinganisha na dawa za kulevya kutoka nje ya nchi ambazo tumezidhibiti," alisema.



Mmiliki wa Taasisi ya Mo Foundation, Mohamed Dewji (MO), akizungumza na wanafunzi mbalimbali jijini Dar es Salaam jana, aliowafadhili kimasomo kupitia taasisi hiyo, baada ya kuhitimu masomo ya vyuo vikuu mbalimbali kwa kuwapa pongezi kwa kujitahidi katika masomo yao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MO Dewji amwahidi Samia ajira 100,000

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Mohamed Dewji 'MO Dewji', amebainisha kufurahishwa na jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kuimarisha uwekezaji na biashara nchini.

Katika kuunga mkono jitihada hizo, MO Dewji ameahidi kuwa katika kipindi cha miaka minne ya utawala wa Rais Samia, ataongeza ajira kutoka 31,000 za sasa hadi 100,000.

Mkurugenzi Mtendaji huyo wa Kampuni ya Mohamed Enterprisses (MeTL), aliahidi hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na baadhi ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaofadhiliwa na Taasisi yake (MO Dewji Foundation).

Alisema Rais Samia amerejesha uhusiano mzuri na mataifa mbalimbali na wawekezaji, jambo analoamini litasaidia kukua kwa uchumi wa taifa, mtu mmoja mmoja na kuongeza ajira.

"Kuna mwelekeo mzuri chini ya Rais Samia, ninawaomba wafanyabiashara wenzangu tumuunge mkono Rais wetu kwa kuwa anataka tupige hatua na kukuza uchumi," alisema.

MO Dewji alisema Rais Samia anafanya vizuri katika kuwavutia wawekezaji wa nje na kuwalinda, hivyo anaamini baada ya miaka michache uchumi wa Tanzania utaimarika zaidi.

Kuhusu ufadhili wa MO Dewji Foundation kwa wanafunzi hao takriban 100, MO Dewji alisema ulianza mwaka 2015 na kadri siku zinavyokwenda ndivyo anavyoongeza zaidi idadi ya wanufaika, akilenga kuwafikia 10,000 katika miaka mitano ijayo.

Aliwataka wanufaika hao kuendelea kumwombea kwa kuwa anapitia wakati mgumu kwenye maisha yake.

"Mimi ninawaomba mkishafanikiwa mkumbuke kuwasaidia na wengine kwa kuwa mimi sitaki mnirejeshee hata senti moja, lengo langu ni kuhakikisha tunapiga hatua na kuondokana na umaskini," alisema.

Bilionea huyo kijana zaidi Afrika, alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo, zaidi ya Sh. bilioni moja zimetumika katika mradi huo wa kuwafadhili wanafunzi vyuoni ili wafikie ndoto zao.

"Uhitaji ni mkubwa lakini tunaangalia zaidi wale wanaotoka katika mazingira magumu bila upendeleo wowote, tunazingatia usawa kijinsia na hata dini," alisema.

Miriam Ibrahim, mmoja wa wanufaika hao, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuwasaidia kufikia ndoto zao.

"Tumekuwa tukipata fursa mbalimbali kupitia taasisi hii ikiwamo wengine kupata kazi katika kampuni ya MeTL. Ninatoa wito kwa taasisi zingine kuiga mfano huu," alisifu.

Baraka Edward, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema: "Tukisema tukulipe kwa kile ambacho umekifanya hatuwezi.

Hata tukisema tuje kufanya kazi bure katika kampuni yako haiwezi kulipa jinsi ulivyotusaidia. Mungu akubariki sana, Asante MO!"

Katika mkutano wake huo na wanafunzi hao, MO Dewji pia alikumbusha kuhusu tukio la kutekwa kwake lililotokea Oktoba 11, mwaka juzi kwenye Hoteli ya Colosseum jijini Dar es Salaam.

"Lazima nimshukuru Mungu, nina deni kubwa na nchi hii. Ninajua mnajua mimi nilitekwa siku tisa, nilikuwa najua nakufa, lakini Watanzania waliniombea na Mungu akawasikia.

"Nina deni kwa Watanzania ndiyo maana sitaacha kujitolea kila nilichonacho kwa ajili yao," MO Dewji alihitimisha.


IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE
NO.68. 2021

In the matter of the Estate of the LATE CHRISTINA PAULO NGHUKU of Mwaja-Dodoma within Dodoma city Council of Dodoma.
And
In the matter of the Application for letters of Administration by IRENE LUCIAN STEPHANO
GENERAL CITATION
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **29 Day of JULY 2021.**
**Dated at Dodoma this 23 day of JULY 2021**
Presented for filling this **23 day of JULY 2021.**

116372502

## HABARI KITAIFA

# Marufuku mikusanyiko Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya amepiga marufuku mikusanyiko ya aina yoyote kufanyika ndani ya mkoa huo ili kuepuka kusambaa kwa maambukizi ya virusi vya corona, akisisitiza kuchukua hatua kali za kisheria kwa yeyote atakayekiuka katazo hilo.

Juma Homera alitangaza katazo hilo jana wilayani Kyela alipozungumza na wananchi wakati wa ziara ya kukagua miradi ya maendeleo.

Aliliagiza Jeshi la Polisi kutekeleza alichokiita kuwashughulikia watu wote watakaofanya mikusanyiko hiyo.

Homera alisema ugonjwa wa corona upo na unagharimu maisha ya watu, hivyo serikali haitakuwa na uvumilivu dhidi ya wanaohamasisha mikusanyiko, akidai wao wameshachanjwa na hawana hofu ya kupata maambukizi.

"Sisi tunazuia maambukizi, tunataka vifaa vya kuwasaidia madaktari kuwahudumia wananchi vizuri, lakini kuna watu wanataka mikusanyiko na mikusanyiko yoyote lazima iwe na kibali, sasa wewe jichanganye huko, tukikufurumisha usije ukalalamika," alionya.

Aliliagiza Jeshi la Polisi kusimamia katazo hilo kwa kuhakikisha watu hawafanyi mikusanyiko katika eneo lolote ndani ya mkoa huo yakiwamo maandamano yanayohamasishwa na baadhi ya vyama vya siasa.

Vilevile, aliliagiza jeshi hilo kuhakikisha watu wote wanaopanda vyombo vya usafiri wa umma, wanavaa barakoa kabla ya kupanda vyombo hivyo na kuhakikisha vyombo hivyo zikiwamo daladala zinabeba abiria kulingana na uwezo wake ili kuepusha misongamano.

Homera pia aliwataka wananchi kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono ili kuepuka maambukizi ya virusi hivyo.

"Mkiangalia hapa mimi na DC (Mkuu wa Wilaya) na viongozi wengine ambao nimeambatana nao, tumevaa barakoa kwa ajili ya kujilinda na tatizo hili, hivyo ninawashauri nanyi mshone barakoa zenu na mzivae, siyo lazima ununuwe, wewe jishonee ya kwako," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Homera alisema ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya, serikali imeongeza wasambazaji wa dawa kutoka mmoja mpaka wanne ili vituo vyote vya kutolea huduma za afya viwe vinapata dawa kwa wakati mkoani humo.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kuunda kamati maalum za kukagua maduka yote ya watu binafsi wanaouza dawa za binadamu ili kubaini kama hakuna dawa za serikali zinazouzwa huko na watakaobainika kuuza dawa hizo, lazima wachukuliwe hatua za kisheria.

"Kumekuwa na tabia ya baadhi ya watumishi wa afya, dawa za serikali zikiingia wanasema mgodi umetema, wanaiba dawa, wanakwenda kuziuza kwenye maduka ya watu binafsi.

"Sasa tutafanya upekuzi mpaka nyumbani kwa watumishi wa afya na tukizikuta lazima tutawajibishana," alihadharisha.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Agelina Lutambi, aliwataka wananchi wa mkoa huo kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (CHF) ili iwasaidie kupata huduma za matibabu kila wanapougua.

Alisema magonjwa huwa hayapigi hodi na wakati mwingine huwa yanakuja wakati ambao mtu anakuwa hana akiba yoyote na hivyo akasisitiza kuwa mfuko huo unasaidia wakati kama huo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi (wa pili kulia), akimkaribisha Balozi wa Marekani nchini, Balozi Donald Wright, ambaye alifanya ziara ya kujionea kazi inayofanywa na hospitali hiyo, mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii, sambamba na kutembelea vitengo na jengo jipya litakalohudumia watoto na kinamama wenye ujauzito hatarishi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango: 'Tumezimiss' busara za Mkapa CCM

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) wanakosa hekima, maoni na ushauri wa Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa.

Dk. Mpango alibainisha hayo jana alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika misa ya kumbukumbu ya mwaka mmoja tangu kufariki dunia kwa kiongozi huyo, iliyofanyika Lupaso, Masasi mkoani Mtwara. Alisema Hayati Mkapa alikuwa mtu anayeipenda familia na taifa, akibainisha kuwa kipindi cha mwaka mmoja bila yeye, mke wake, watoto wake, wajukuu na wamekosa kupata nasaha, busara na malezi waliyozoea kuyapata wakati wa uhai wake.

"Serikali, CCM na taifa kwa ujumla tumekosa kupata hekima, maoni na ushauri katika masuala mbalimbali ya kitaifa na hata taasisi mbalimbali kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Mkapa Foundation (Taasisi ya Mkapa) zinaona pengo kubwa alilotuachia," alisema.

Makamu wa Rais alisema Rais Mkapa alikuwa na mchango mkubwa kwenye mageuzi ya kiuchumi, mapambano dhidi ya rushwa ambayo yalisababisha Tanzania kumpa jina la 'Bwana Msafi'.

Alisema mapambano yake dhidi ya UKIMWI, kuhimiza uwazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma na usuluhushi wa migogoro ya kisiasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi na Kenya, ni alama zisizofutika alizoziacha.

"Wasifu wa Hayati Mkapa umejaa sifa lukuki na kazi nyingi nzuri alizozifanya. Pamoja na mambo mengine Mwenyezi Mungu alimjalia kipawa cha uongozi na uwezo mkubwa wa kunena na kutenda yote aliyoamini kuwa ya manufaa kwa taifa na watu wake," alisifu.

Alisema amechagua mambo machache ya kujifunza kutokana na maisha, utumishi na uongozi wake ambapo alichagua kuishi kwa sala na kazi, alikuwa mkatoliki hodari na alikuwa hakosi kushiriki ibada.

"Alijitolea kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo ya kanisa lake na madhehebu mengine ya kikristo hata dini nyingine, hata hivi leo mara baada ya ibada hii, kutakuwa na ufunguzi wa nyumba ya mapadre wa Lupaso ambayo Hayati Mkapa aliikarabati, ninashukuru familia kwa kuendeleza kazi nzuri aliyoanzisha," alisema.

Dk. Mpango alisema kutoka kwake wanajifunza wito kwa kila Mtanzania kujitoa nafsi kwa kufanya kazi ambapo bila shaka Hayati John Magufuli, Rais wa awamu ya tano, alichota hiyo kwa Mkapa.

Akiwasilisha salamu za Rais Samia, Dk. Mpango, alimnukuu Mkuu wa Nchi akisema: "Ninakutuma uwapelekee salamu zangu za upendo wanafamilia, wana Lupaso, ndugu, jamaa na rafiki na wananchi wote kwa ujumla.

"Ninawahakikishia serikali itaendelea kumuenzi baba yetu na kiongozi wetu, Hayati Benjamini William Mkapa."

Askofu Mkuu mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Kardinali Polycarp Pengo, alisema Mungu amewakutanisha kutafakari fumbo la kifo cha mwanadamu.

"Swali linalohitaji jawabu lakini swali ambalo linabaki katika kipindi chote cha maisha ya mwanadamu, watu wanaweza kufanya mambo makubwa kwa ajili ya wanadamu wenzao lakini tunajiuliza kazi yote hiyo waliyofanya baada ya kifo chao ina maana gani.

"Ni kitu gani kinabaki cha manufaa pamoja na jasho jingi wanaloweza kuwa wametiririsha kwa ajili ya manufaa ya watu wengine, na wengine kwa damu nyingi walizomwaga kutoka kwa watu wengine kwa ajili ya sifa na utukufu wao, mwisho wake una maana gani? Na ni swali ambalo tunajiuliza siku ya leo," alisema.

Alisema wanamshukuru Mungu kwa zawadi ya Hayati Mkapa kwa taifa kwa sababu amefanya taifa kupitia yeye lijulikane kwa watu wengine.

# Tanzania yakamilisha rasimu kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, amesema Tanzania imekamilisha rasimu ya Mchango wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Nationally Determined Contributions -NDCs).

Mary alibainisha hayo juzi jijini Dodoma katika hotuba ya ufunguzi wa kongamano kuhusu Mchango wa Taifa katika Upunguzaji wa Uzalishaji wa Gesijoto (NDC) iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Mazingira, Dk. Andrew Komba. Alisema mchango wa NDC umetokana na Mpango wa Ahadi za Kitaifa (Intended Nationally Determined Contributions-INDCs) za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi uliowasilishwa na Tanzania katika Sekretarieti ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi Septemba 2015. W"Kama mnavyofahamu, nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania zinaathirika sana na mabadiliko ya tabianchi kutokana na uwezo mdogo kifedha na kiteknolojia kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. "Kutokana na ukweli huo, kuhimili mabadiliko ya tabianchi ndiyo kipaumbele cha nchi hizi," alisema.

Katika hotuba yake hiyo, Mary alisema nchi zinazoendelea kutokana na kutokuwa na viwanda vingi, hazijachangia au zimechangia kidogo katika uzalishaji wa gesijoto ambazo zinasababisha au zimesababisha mabadiliko ya tabianchi.

RIPOTI MAALUM

# Miaka 44 safari kupanda na kuporomoka kwa ATCL

- Watumishi wake walipana mabilioni
- Samia: Vyovyote vile haitaachwa
- Yainuliwa na ndege 9, tatu zinakuja

**Na Sanula Athanas**

NDANI ya Ukumbi wa Bunge wanasiasa kwa miaka mingi wamekuwa wakisikika wakimwita njiwa, sasa bado wanamwita njiwa na wajao huenda wataendelea kumwita hivyo hivyo.

Ni jina ambalo wabunge walimebatiza Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), watunga sheria hao wakigawanyika katika makundi mawili ya wanaotaka shirika liendelezwe na upande wa pili ni wa wanaodai lifutwe.

Shida ni nini? Chimbuko la mjadala ni shirika kuendeshwa kwa hasara ya mabilioni ya shilingi tangu zama za uongozi wa Rais Ali Hassan Mwinyi, sasa likiripotiwa kutengeneza hasara ya Sh. bilioni 472.853 huku watumishi wake wakilipana posho za mabilioni kinyume cha sheria.

Haiba ya kiwango hicho cha hasara kilichotajwa inatisha, lakini kiulizo kinajitokeza tena; nini mzizi wa tatizo, imekuwaje kufikia kiwango hicho na kama kuna lawama, inauangukia upande upi na kwa vipi?

Inaenda mbali kwamba mzigo huo wa hasara na udhibiti wake unakabiliwa kwa namna gani?

Ni maswali yasiyohitaji majibu ya kukurupuka, bali tafakuri ya kina na busara iliyotukuka, kutathmini undani na hatima ya mustakabali uliokwishafikiwa na shirika liendako, ili kuendelea kulishuhudia likisimama katika mazingira chanya kwa manufaa ya nchi.

Imeshatimu miezi miwili na wiki kadhaa tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipolihutubia Bunge jijini Dodoma na kuweka wazi ATCL itabaki kuwa mali ya umma, pia kwa manufaa ya umma.

Hata kabla yake, Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, Kassim Majaliwa, alidokeza azma ya kiserikali kuendeleza maboresho ya ATCL kwa kuipanulia mtaji.

Majaliwa ambaye pia ni Waziri Mkuu nchini, alibainisha kwamba hilo linafanyika sambamba na ununuzi wa ndege mpya zikiwamo tatu ambazo mustakabali wa malipo tayari uko katika bajeti ya sasa.

Hoja ya kuwa na ATCL endelevu pia imepata ushawishi wa kumuunga mkono Waziri Mkuu Majaliwa, ingawaje kuna kundi dogo lingine la wabunge halikubaliani nayo kwa madai shirika halihitajiki tena.

Kundi dogo hilo linaundwa na wabunge kutoka vyama vya upinzani na wachache kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambao msingi wa hoja yao umezama kwenye dhana kwamba ununuzi wa ndege ya kufufua ATCL ni sawa na kuwekeza kwenye maendeleo ya vitu badala ya maendeleo ya watu.

Je, ATCL ya leo inayobeba mjadala, msukosuko wake huo umeanzia wapi? Shirika hilo ambalo awali lilitwa ATC, lilizaliwa mwaka 1977 kutokana na kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambayo moja ya taasisi zake tanzu ni lililokuwa Shirika la Ndege la Afrika Mashariki (EAA).

Ndani ya mgawanyo wa mali za EAC, kupitia mali za EAA, ndipo ikazaliwa ATC.

Hata hivyo, mgawanyo rasmi kisheria wa mali za EAC ulifanyika wastani wa mwaka mmoja tangu kuzaliwa kwa ATC.

Mwanzoni ATC ilianza kazi ikiwa na ndege moja ya kwake, sambamba na nyingine za kukodi. Ilipofika wakati wa mgawo, ATC iliambulia ndege moja aina ya Twin Otters yenye uwezo wa kubeba abiria 19.

Ndani ya muda mfupi, mwishoni mwa mwaka 1978, ATC ilipiga hatua kubwa kwa kununua ndege mbili mpya aina ya Boeing 737 zenye uwezo wa kubeba abiria 103 kila moja.

Zikiwa zimeng'arisha sifa ya nchi, pia shirika lenyewe, ndege hizo mpya zilipewa majina ya Kilimanjaro na Serengeti, viashiria vilivyoonyeshwa kwenye alama zake za mkia.

Mwaka 1980, ATC ilijitanua zaidi kwa kununua ndege nne aina ya Fokker Friendship, zenye uwezo wa kubeba abiria 44 kila moja.

Ni hatua iliyozidi kuivumisha ATC, iliyoendana na kuwapeleka mafunzoni Uholanzi wahitimu wapya wa elimu ya sekondari kwa ajili ya ufundi na urubani.

Ulikuwa mwaka wa ATC kujitanua, kwani mwaka huo huo (1980) ilinunua ndege nne aina ya Twin Otters zenye uwezo kama ile iliyotajwa awali.



Moja ya ndege zilizonunuliwa na ATC mwaka 1978. **PICHA: MAKTABA**

**ZAMA ZA MWINYI**

1985 ni mwaka ulioandika historia mpya kitaifa, kustaafu kwa Mwalimu Julius Nyerere, aliyeshika usukani tangu uhuru na taifa, hali kadhalika mfumo hodhi wa siasa na uchumi tangu mwaka 1964, vyote vilikabiliwa na mabadiliko.

Ikawa ni zama mpya, Tanzania chini ya Rais Mwinyi, siasa na uchumi wa nchi nazo kuhamia kwenye mfumo huria, ambao matokeo yake kwa ujumla yalishuhudia mabadiliko makubwa kitaifa na baadhi ya maeneo hayakubaki salama.

Kwa kuwa uchumi wa nchi uliingia katika mfumo mpya, uzoefu, uwekezaji na kutomudu ushindani ni miongoni mwa mambo yaliyosababisha maporomoko makubwa katika maeneo husika, ATC na taasisi zingine za umma zilitikisika.

Mpasuko huo ndiyo Rais Mwinyi, maarufu Mzee Rukhsa, jina alilobatizwa kutokana na itikadi yake ya kiuchumi wakati huo, anakiri iliweka njiapanda ATC na baadhi ya mifumo mingine ya kiuchumi.

Rais Mwinyi anasimulia mkasa wa ATC kwamba kuanzia waamuzi wa kiserikali - wabunge waliitaka serikali yake ipunguze matumizi yasiyo ya lazima.

Anasema alilazimika kuchukua uamuzi mgumu ukiwamo wa kutowaajiri wahitimu wote wa vyuo vikuu, suala lililokuwa geni wakati huo, kwani wahitimu wote walikuwa wanaajiriwa moja kwa moja.

Anasimulia namna rungu la uamuzi mgumu lilivyowadondokea watumishi 310 wa ATC ambao alilazimika "kuwafuta kazi" ili kupunguza mzigo wa malipo ya ujira wao.

Rais Mwinyi anabainisha hayo kwenye kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', akikiri ATC ilikuwa inasuasua, hata ofisi zake sita ndani na nje ya nchi zikafungwa.

Anasema ni zama ambazo ATC na mashirika mengine ya umma yalizalisha hasara ya Sh. bilioni 46 katika mwaka mmoja pekee (1992/93).

Anafafanua: "Ukaguzi wa mashirika ya umma wa mwaka 1992/93 uliofanywa na Shirika la Ukaguzi Tanzania, ulionesha kuwa miongoni mwa mashirika 345 yaliyokaguliwa, yalikuwapo machache yaliyopata faida ya Sh. bilioni 51.2 kabla ya kodi, lakini mengi (ikiwamo ATC) ni yale yaliyopata hasara ya jumla ya Sh. bilioni 97.2.

"Kwa maneno mengine, kwa ujumla wao waliitia serikali hasara ya Sh. bilioni 46 kwa mwaka mmoja tu kwa thamani ya fedha ya wakati huo."

**ATCL YA SAMIA**

Rais Samia naye anakiri ATCL ya sasa bado inaogelea kwenye dimbwi la hasara ingawa dira yake ya kiuongozi ni kwamba inahitaji uwekezaji mkubwa, kulelewa na safari ya neema iendapo bado ipo.

Akilihutubia Bunge jijini Dodoma Aprili 22 mwaka huu, Rais Samia aliahidi kulinusuru shirika hilo, akisisitiza serikali yake haitakuwa tayari kuliona linaendelea kutengeneza hasara.

Alisema mikakati yake inajumuisha kuliwezesha kwa rasilimali ili liendeshwe kwa weledi na stadi za kibiashara zitakazohimili mikiki ya soko, huku akikiri biashara ya usafiri wa anga ni ngumu.

"Shirika limekuwa likijiendesha kwa hasara, lakini hii ni kwa sababu lilirithi madeni makubwa. Hivyo, serikali inabidi kuweka mikakati ya kulipeleka mbele," alisema.

INAENDELEA UK. 5

RIPOTI MAALUM

# Miaka 44 safari kupanda na kuporomoka kwa ATCL

INATOKA UK. 4

Rais Samia pia alitaja mkakati anaoufanyia kazi unajumuisha nafuu ya kodi katika baadhi ya maeneo, hali kadhalika namna ya kuipa ATCL nafuu ya mzigo wa kodi iliyonao.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu Majaliwa, aina ya ndege zilizoko njiani kufika nchini ndani ya mwaka wa fedha uliopo, mbili kubwa aina ya Airbus. Hata hivyo, hakutaja uwezo wake.

Ndege ya tatu ni aina ya Dash 8-Q400 De-Havilland, zote zitakapotua nchini zitaifanya serikali kuwa na jumla ya ndege mpya 12 ambazo zinatumiwa na ATCL.

Hadi sasa shirika hilo katika maboresho yake mapya lina safari za kwenda katika baadhi ya nchi ambako Tanzania ina uhusiano wa karibu zikiwamo China na India.

### KUTOKA KWA CAG

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20, inataja serikali ilitumia jumla ya Sh. trilioni 1.028 kununua ndege nane kati ya tisa zilizonunuliwa awali.

Vilevile, CAG Charles Kichere, anabainisha ndani ya miaka mitano ya ATCL, kati ya 2015/16 na 2019/20, shirika lilipatiwa ruzuku ya Sh. bilioni 153.711.

CAG anasema ndani ya kipindi hicho, ATCL ilipata hasara ya Sh. bilioni 153.542; huku ndani ya mwaka mmoja wa fedha (2019/20), ikipata hasara ya Sh. bilioni 60.246.

Vivyo hivyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu huyo anasema katika mwaka wa fedha 2018/19, mapato ghafi ya ATCL yalikuwa Sh. bilioni 112; na katika mwaka uliofuata, yaliongezeka na kufika Sh. bilioni 158, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 46, ambayo ni ziada ya asilimia 41.

Haiba nzuri ya kuongezeka mapato ya ATCL, kwa upande wa pili ilichafuliwa na ongezeko la matumizi yake kutoka Sh. bilioni 134 mwaka 2018/19 hadi Sh. bilioni 193 mwaka uliofuata. Ni ziada ya matumizi Sh. bilioni 59 au asilimia 45.

Hapo kuna maana gani? Katika mwaka wa fedha 2018/19, wakati wa matumizi ya juu kwa Sh. bilioni 134, ATCL iliambulia mapato ya Sh. bilioni 112, ikiangukia hasara ya Sh. bilioni 22.

Hali kadhalika, mwaka uliofuata (2019/20) matumizi yalikuwa Sh. bilioni 193 wakati mapato yaligota kwenye Sh. bilioni 158, ukawa ni mwaka mwingine wa hasara ya Sh. bilioni 35.

Yote hayo kwa ujumla yakaifanya ATCL katika miaka hiyo miwili kupata hasara ya jumla ya Sh. bilioni 57.

### KUFURU YA POSHO

CAG Kichere anabainisha kuwa Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Mapato ya Mwaka 2014 kiliondoa posho za nyumba, usafiri, madaraka, kufanya kazi saa za ziada, kufanya kazi katika mazingira magumu na honoraria kwa mtumishi wa serikali au taasisi ambayo bajeti yake hulipwa yote au kwa kiwango kikubwa na ruzuku za serikali.

Hata hivyo, CAG anasema alibaini kuwa katika mwaka fedha 2019/20, ATCL ililipa jumla ya posho za Sh. bilioni 1.11 na kwamba posho hizo zililipwa bila kutoza kodi ya mapato.

Uhalisia wake ni sawa na wastani wa posho ya Sh. milioni 1.93 kwa kila mtumishi wa ATCL kwa mwaka. Ripoti ya CAG inabainisha shirika lina watumishi 575.

"Nilibaini kutokata kodi ya mapato katika posho hizo kulisababishwa na kutokuwa na ujuzi wa kutosha juu ya matumizi ya Sheria ya Kodi ya Mapato kwa watumishi ambao wanashughulika na posho na malipo ya mishahara. Hii inapelekea serikali kupoteza mapato na ATCL inaweza kupata adhabu na riba zisizo za lazima kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)," abainisha.


Kwa mujibu wa CAG Kichere, hadi kufikia mwaka huo wa ukaguzi (2019/20), ATCL ilikuwa na mtaji hasi wa Sh. bilioni 472.853.

Katika mtazamo huo wa matumizi, CAG ana angalizo la baadhi ya maeneo kwamba ni sehemu ya mzizi wa gharama kubwa unaoishia kwenye lalamiko kuu la hasara na madeni.

Mosi; anataja gharama za usafirishaji mizigo na abiria ziko juu kuliko mapato yake.

Pili; gharama ziliangukia kwenye matumizi ya kiutawala ikiwamo malipo ya stahiki za wafanyakazi yasiyoendana na kanuni na miongozo rasmi.

"Ni maoni yangu kuwa bila kudhibiti gharama za uendeshaji pamoja na za kibiashara, kampuni (ATCL) itaendelea kupata hasara," anahitimisha CAG Kichere.




Posho za watumishi wa ATCL zilizolipwa kinyume cha sheria bila kukatwa kodi. **CHANZO: Ripoti ya CAG 2019/20**

### HOJA ZA ATCL

Siku mbili baada ya Rais Samia kutoa angalizo lake bungeni kuhusu ATCL, mnamo Aprili 24, mwaka huu, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, akakutana na uongozi wa shirika hilo kutaka ufafanuzi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Albinus Manumbu, anajitetea dhidi ya hoja hizo akiwa na angalizo la mambo mawili, ambayo yako nje ya uwezo wao.

"Hizi ndege ambazo ATCL inaziendesha, ni mali ya serikali na anayezimiliki ni Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA). Shirika linawajibika kulipa kodi, jambo ambalo ni mojawapo ya gharama za uendeshaji," anasema.

Manumbu pia anataja maudhui ya mkataba uliopo kati ya ATCL na TGFA siyo rafiki kwa shirika hilo la ndege kuelemewa na mzigo wa gharama.

Anatoa mfano kati ya Machi na Juni mwaka jana, Tanzania na kwingineko duniani wameumia kiuchumi kutokana na janga la corona, bado ATCL iliendelea kulipa kodi za ukodishaji ndege, ilhali haikuwa ikizalisha kibiashara.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu huyo anaongeza kwamba kuwapo riba ya Sh. bilioni 16 itokanayo na madeni endelevu tangu shirika hilo kuzaliwa, sambamba na gharama kubwa za kesi zinazoihusu taasisi hiyo, kumekuwa kukiwaumiza.

Naibu Waziri Waitara amejumuisha hoja hizo kwa kuiagiza menejimenti ya ATCL kurekebisha dosari, ili kuweka mazingira sahihi ya kutekeleza ahadi ya Rais Samia, kuchukua hatua za maboresho.



Kiongozi Mkuu wa ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe



Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) Halima Mdee

### WANENAVYO WADAU

Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), anarejea ripoti mbili zilizotolewa na CAG Ludovick Utouh na CAG Profesa Mussa Assad, zote zikiwa na maoni kwamba ATCL itangazwe kuwa mfilisi ili kuepuka madeni iliyonayo.

Utouh alikuwa CAG kwa miaka minane kuanzia 2006 hadi 2014 alipokabidhi kiti kwa Profesa Assad aliyeendelea nacho hadi Novemba 3, 2019.

Katika hoja yake, Mdee aliyekuwa Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, katika Bunge la 11, anafafanua kuwa hasara inayolalamikiwa sasa ATCL, ni matokeo ya kutofanyiwa kazi kwa ushauri wa CAG Utouh na Profesa Assad.

"CAG Utouh alitoa mapendekezo 15 kuepuka hasara ATCL, serikali iliyapuuza. Profesa Assad katika mwaka wake wa kwanza wa uongozi kwenye ofisi hiyo, alitoa ripoti iliyobainisha ATCL ilikuwa imetengeneza hasara kwa miaka 10 mfululizo na akatoa mapendekezo mazuri, yakapuuzwa.

"Sasa CAG Kichere anasema shirika limetengeneza hasara ya Sh. bilioni 472, tulipaswa kumtangaza njiwa wetu (ATCL) kuwa mfilisi ili kuepuka haya," Mdee analalamika.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, anasema kinachohitajika sasa ni kufanya anachokiita uamuzi sahihi unaojumuisha kubadili muundo wa umiliki wa ATCL.

Zitto ambaye kitaaluma ni mchumi, anasema kuna haja muundo huo ubadilishwe kwa kuhusisha mashirika ya uhifadhi na utalii kama wamiliki.

"TANAPA (Shirika la Hifadhi za Taifa) na NCAA (Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro) wamilikishwe asilimia 60 ya shirika na hivyo waondolewe katika orodha ya mashirika ya kupeleka Hazina asilimia 15 ya makusanyo yao ghafi.

"Vilevile, mashirika haya ya utalii yaachiwe kujiendesha na kukusanya mapato yao wenyewe.

"Asilimia 40 zilizobaki zimilikiwe na serikali ambapo shirika likikaa vyema, asilimia 25 ya shirika wamilikishwe wananchi kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam, ili kuongeza uwazi na kuboresha misingi bora ya uendeshaji wa shirika," Zitto anashauri.

Wakati serikali ikiweka mikakati kuepuka hasara, Chama cha Kimataifa cha Usafiri wa Anga (IATA) kinatahadharisha kuwa mashirika ya ndege mwaka huu yanatarajiwa kupata hasara ya jumla ya Dola za Marekani bilioni 47.7.

IATA inabainisha kuwa kiwango hicho cha hasara kinatarajiwa kuongezeka kutoka hasara ya Dola bilioni 38 iliyoripotiwa mwaka jana, sababu kubwa ikiwa ni mlipuko wa virusi vya corona.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utashi wa kisiasa muhimu mapambano dhidi ya corona

**SERIKALI** kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imebainisha kwamba hali ya maambukizi ya corona nchini, inaendelea kuwa mbaya kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo baadhi ya watendaji wanaopaswa kutimiza wajibu wao kisheria, kutokufanya hivyo.

Licha ya watendaji kutupiwa mzigo, wizara kupitia Waziri wake, Dk. Dorothy Gwajima, kama alivyokaririwa na vyombo na vyombo vya habari, alisema juzi kuwa sababu nyingine ni Watanzania kutozingatia afua zilizowekwa katika kujikinga na janga hilo ambalo kwa sasa limetamalaki katika dunia kwa awamu ya tatu.

Afua hizo ni kuvaa barakoa, kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka, kutumia vipukuswa na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Waziri alitoa takwimu zinazoonyesha kuwa idadi ya wagonjwa wa corona imefika 682 kutoka wagonjwa wa awali 408. Kati yao, 284 walikuwa wanapumua kwa msaada wa mashine kufikia Julai 21 mwaka huu.

Kutokana na hali hiyo, waziri alisema katika kuhakikisha mapambano dhidi ya ugonjwa huo yanafanikiwa, serikali haitawavumilia viongozi ambao hawatimizi wajibu wao na kwamba itaimarisha ufuatiliaji na kuwabana wale wasiotimiza wajibu wao.

Wakati serikali ikitanabaisha hivyo, taarifa zinabainisha kwamba ugonjwa huo unazidi kusambaa katika mikoa mbalimbali nchini na kusababisha watu kulazwa na baadhi kupoteza maisha.

Mkoani Kilimanjaro, kwa mfano, Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC imeelezewa kuzidiwa wagonjwa wenye matatizo ya kupumua huku akibainishwa kuwa hata mitungi ya oksijeni kwa ajili ya wagonjwa wenye tatizo hilo inapungua. Hospitali hiyo ina uwezo wa kutengeneza mitungi 400 kwa siku na kwamba matumizi yake kwa siku kutokana na ongezeko la wagonjwa ni 400 pia.

Licha ya Kilimanjaro, mikoa mingine ambayo imeelezwa kuwa na maambukizi makubwa ni Dar es Salaam, Iringa, Arusha, Mwanza, Dodoma na Tanga. Idadi kubwa ya mikoa hiyo ni ile yenye watu wengi na maingiliano ya kibiashara.

Kama alivyoelezwa Waziri Gwajima, kasi ya maambukizi hayo inatokana na ulegevu katika ufuatiliaji na udhibiti na kufuata afua kama inavyotakiwa, ni kweli tahadhari inachukuliwa kwa kiasi kidogo kulinganisha na awamu zilizopita. Jijini Dar es Salaam, kwa mfano, watu hawachukui tahadhari katika mikusanyiko kama vile kwenye masoko, viwanja vya michezo na kwenye mabasi.

Pamoja na hayo, inatia moyo kwamba wakuu wa mikoa ya Mbeya, Tanga, Arusha na Mwanza wameanza kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku mikusanyiko isiyo ya lazima. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika kuhakikisha watu wanajikinga dhidi ya ugonjwa huo ambao ni tishio si tu kwa Tanzania bali kwa Afrika na dunia nzima.

Ili kuhakikisha tatizo hilo linadhibitiwa ipasavyo, ni vyema serikali ikatangaza watu kukaa kwenye viti na asiwapo mtu wa kusimama kwenye mabasi huku kila mmoja akivaa barakoa akiwa katika chombo cha usafiri na mikusanyiko.

Mwaka jana, mathalan, uongozi wa mkoa wa Dar es Salaam ulitoa agizo kama hilo na kufanikiwa kudhibiti corona kwa kiwango kikubwa, hivyo ni imani kwamba mpango kama huo utasaidia katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo kwa sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Meza ya maridhiano itumike kuleta mwafaka wa kisiasa

Na Sabato Kasika

**CHAMA** cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), hakikufanikiwa kutimiza msimamo wake na kufanya mikutano na makongamano ya kudai katiba mpya nchi nzima bila kujali maelekezo ya serikali.

Hakikutimiza msimamo huo ambao kiliutoa wiki iliyopita baada ya kuzuiwa na vyombo vya dola, huku kikiwa kimejipanga kuanza mikutano hiyo jijini Mwanza na kisha kingeendelea katika mikoa mingine.

Kupitia kwa mwenyekiti wake wa taifa, Freeman Mbowe, CHADEMA ilitoa msimamo huo, huku vyama vya siasa vikiwa vimeruhusiwa kufanya mikutano ya ndani tu, hali ambayo huenda ingesababisha sintofahamu.

Mwenyekiti huyo alieleza sababu ya msimamo huo kuwa ni kukwaza uamuzi wa Jeshi la Polisi kuzuia kufanyika kwa kongamano la kwanza la katiba mpya na kuwashikilia wafuasi wake jijini Mwanza.

Mbowe alisisitiza kuwapo kwa katiba mpya ambayo Rais Samia Suluhu Hassan alishaitolea ufafanuzi kwa kuwataka wadau na Watanzania kwa ujumla, wausubiri kwanza aimarishe nchi kiuchumi.

Pamoja na kuwataka wasubiri aimarishe nchi kiuchumi, pia Rais aligusia suala la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa iendelee kuwa ya ndani badala ya ile ya hadhara ambayo viongozi wa vyama hivyo wamekuwa wakitaka.

Viongozi wa chama hicho wamekaa na kutafakari, kisha wakaja na uamuzi huo, lakini pamoja na hayo, bado kuna haja ya kutafakari zaidi ili kufikia muafaka mzuri ambao hautasababisha uvunjifu wa amani.

> **Viongozi wa chama hicho wamekaa na kutafakari, kisha wakaja na uamuzi huo, lakini pamoja na hayo, bado kuna haja ya kutafakari zaidi ili kufikia muafaka mzuri ambao hautasababisha uvunjifu wa amani.**

Lakini pia, si vibaya kuendelea kuvuta subira, ili ahadi za Rais ikiwamo ya kukutana na vyama vya upinzani katika meza ya maridhiano, kwa lengo la kuweka vizuri mambo ambayo wanaamini hayako sawa.

Hatua kama hiyo ni muhimu kwa taifa la Tanzania, badala ya kutaka kufanya siasa kwa njia ambayo wakati mwingine inaweza kusababisha wakaingia katika mvutano na serikali, jambo ambalo lingeishia kwenye meza ya maridhiano.

Binafsi ninadhani kwamba, kama Rais angekataa suala la katiba mpya au kutokutana na viongozi wa vyama vya upinzani, ndipo wangeweza kulalamikia hali hiyo, lakini ameonyesha wazi kuwa ana nia njema.

Kwa hali hiyo, ingependeza iwapo wataendelea kusubiri ahadi ya kukutana nao, ili wajadili kwa kina mustakabali wa siasa za Tanzania kwa manufaa ya Watanzania badala ya msimamo wa sasa.

Meza ya maridhiano huwa ina nafasi kubwa ya kumaliza tofauti zozote zikiwamo za kisiasa, hivyo ingekuwa vyema suala la kukutana likapewa uzito, kuliko kuchukua hatua nyingine tofauti na hizo. Ni vyema kuvuta subira, hasa kwa kuzingatia kwamba, Rais ameshakubali uwepo meza ya maridhiano ya vyama vya siasa ili kujenga nyumba moja ambayo ni mama Tanzania.

Lakini CHADEMA wakumbuke kuwa, wanaweza kufanya hayo yanayokusudia kwa lengo zuri, lakini ni vyema wakatambua kuwa, kwenye msafara wa mamba, kenge huwa hawakosekani.

Katika mikutano na makongamano hayo, wanaweza kujitokeza watu wenye nia mbaya na kuanzisha vurugu au kufanya lolote baya na hivyo kujikuta chama chao kinaingia kwenye matatizo.

Kwa mazingira kama hayo, ni vyema chama hicho kikajipa muda zaidi wa kutafakari msimamo huo ambao kwa namna moja au nyingine unaweza ukakisaidia ama kuharibia taswira mbele ya umma.

Ikumbukwe kuwa siasa za maridhiano ni chachu ya amani na pia kila raia ana haki ya kushiriki katika siasa na fursa sawa za kijamii, hivyo msimamo zaidi ungeelekezwa kwenye meza ya maridhiano.

Kimsingi ni kwamba, siasa si uadui, hivyo zisipewe nafasi ya kuwagawa Watanzania, bali pale unapotokea mkwamo, ni vyema wahusika kukaa kwenye meza ya maridhiano, ili kuweka mambo sawa.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Rais somo la ‘managing diversity’ kwa wateule wako sasa linahitajika



**Na Pascal Mayalla**

JAPO chakula ni uhai, kuna msemo usemao: “Mtu hataishi kwa mkate tu”. Vivyo hivyo, nchi zinaendeshwa na kutawaliwa kwa mujibu wa katiba, sheria, taratibu na kanuni, lakini ili kupata maendeleo ya kweli, maendeleo endelevu yenye amani, utulivu na utangamao, maendeleo ya kweli hatayaletwa na sheria na katiba pekee, bali pia ushirikishwaji na kujikubali tuko watu tofauti, lakini bado tu wamoja. Kwa mantiki hiyo, hawa wanaotaka kujadili katiba mpya, kutwa kucha, waachwe tuu ni haki yao.

Makala ya leo, ni kuendesha somo liitwalo “Managing Diversity” kwa baadhi ya viongozi wetu.

Tanzania bado tunakabiliwa na tatizo kubwa la uwapo wa ugonjwa wa “political diversity”, unaosababisha “political hostilities” na unaohitaji tiba ya “political tolerance” kuanzia kwenye mihimili ya Bunge, Serikali na Mahakama. Kuanzia ngazi ya kitaifa, mikoani, wilayani, majimboni, kwenye kata hadi mitaani ambako baadhi ya viongozi wetu wameshindwa kuzitawala tofauti zetu za kisiasa, sasa tunaingia tena katika kukamatana, kuswekana ndani kuonyeshana nguvu ya dola!. Hatutafika salama!.

Rais Mama Samia, ameruhusu mikutano ya ndani ya kisiasa ya vyama vyote.

Viongozi wa kitaifa wa vyama wako huru kuhudhuria mikutano yote ya ndani.

Hoja kwenye mikutano hiyo, ni hoja zozote za ndani kwao, ikiwamo ya katiba mpya.

Tuwavumilie, tuwaache, tujikubali sisi Watanzania ni tofauti kisiasa, kiuchumi na kijamii. Lakini bado tu wamoja kama Watanzania. Hakuna sababu kuanza tena kukamatana na kuswekana lupango. Tanzania ya Mama Samia, siyo Tanzania hiyo!

Tatizo hili linaweza kumalizwa kwa somo la “Managing Political Diversity” ambalo Rais Samia ameshalianza kwa kuwakaribisha wapinzani kwenye shughuli la kitaifa na kuwaalika baadhi ya viongozi wa baadhi ya vyama vikuu vya upinzani Ikulu.

Lakini somo la “Political Tolerance” bado linahitajika sana wakati huu kuliko wakati mwingine wowote, hivyo kunahitajika kuendeshwa kwa somo la “Managing Political Diversity” ya hali ya juu kwa viongozi wa pande zote-serikali, CCM na vyama vya upinzani, asasi za kijamii ili kuonyesha tunataka kujenga Tanzania moja, yenye nia moja, lengo moja na taifa moja moja licha ya tofauti zetu za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hili likifanyika, Rais Samia atabarikiwa sana.

Nchi yetu itabarikiwa sana kwa kupata amani, utulivu na ustawi utakaoleta maendeleo makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Wapinzani wavumiliwe, hoja yao ya kutaka katiba mpya ni ya msingi.

Mikutano ya kisiasa iliyoruhusiwa na katiba iruhusiwe ila iendeshwe kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni.

Naomba kutolea mfano kilichotokea Zanzibar kabla ya mwaka 2010. Ilifika hatua watu wakawa hawasalimiani, hawatembeleani na hata kwenye shida na raha hawashirikiani hadi ikafikia hawazikani! Wanzanzibari wakaamua kuzika tofauti zao, wakashikana mikono wakamua kuwa wamoja. Wakabadili katiba yao na kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) au kwa Kiingereza GNU.

Mabadiliko yale yaliyounda SUK, japo yalikwenda kinyume cha katiba ya Jamhuri ya Muunganowa Tanzania mwaka 1977, kwa katiba ya Zanzibar kuitambua Zanzibar kama nchi na kuihesabu Zanzibar ni moja ya nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati kwa mujibu wa Katiba ya JMT ya mwaka 1977, Tanzania ni nchi moja ya Jamhuri ya Muungano, yenye sehemu mbili, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani au Tanzania Zanzibar.

Kwenye Katiba yetu, Zanzibar inaelezwa si nchi bali ni sehemu ya JMT yenye utawala wake wa ndani.

Enzi hizo ilikuwa Awamu ya Nne chini ya Jakaya Kikwete, ambaye ndiye mwuasisi wa viongozi kuwa na ngozi mgumu. Mabadiliko hayo ya Katiba ya Zanzibar, maadam hayatuhusu, ila yanawahusu Wanzanzibari, yaliachwa hivyo hivyo yalivyo mpaka leo, mpaka kesho. Kule Zanzibar yamo kwenye katiba yao, huku Tanzania hayamo kwenye katiba yetu, lakini kwa vile yameleta maelewano, amani, utulivu na mshikamano, tumeyavumilia, tumeyaacha.

Kuna Watanzania wanataka katiba mpya, waachwe wajadili katiba watakavyo. Waachwe wahamasishane kuhusu katiba mpya.

Watakavyo waachwe wafanye semina, warsha, mikutano na makongamano ya katiba nchi nzima hata kila siku, siku nzima, usiku na mchana, wiki nzima, mwezi mzima, hata mwaka mzima, maadam hawaharibu amani na utulivu uliopo. Waachwe, maana wenzetu muda huo wanao.

Tukubaliane kuwa Tanzania ni nchi ya vyama vingi na kuwatendea haki vyama vyote kutasababisha Rais Samia kubarikiwa, serikali yake kubarikiwa, chama chake CCM kubarikiwa na nchi ya Tanzania kubarikiwa.

Mungu Mbariki Rais wetu Samia afikishe somo la ‘Managing Political Diversity’ kwa serikali yake ili tuwe na ‘Political Tolerance’. Mungu ataibariki Tanzania, atambariki Rais Samia na serikali yake,

**Mungu ibariki Tanzania.**

**0754 270403**
**pascomayalla@gmail.com**

**Rais Mama Samia, ameruhusu mikutano ya ndani ya kisiasa ya vyama vyote. Viongozi wa kitaifa wa vyama wako huru kuhudhuria mikutano yote ya ndani. Hoja kwenye mikutano hiyo, ni hoja zozote za ndani kwao, ikiwamo ya katiba mpya.**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania tumeamua kumkumbatia UVIKO?



**Na Joseph Kulangwa**

UKO nyumbani na mgeni wako mnaangalia luninga, mara linapita tangazo la habari kwa ufupi, habari inaanza na Waziri wa Afya, Dk Dorothy Gwajima, anasema wagonjwa 29 wa UVIKO-19 wamepoteza maisha.

Habari inayofanana na hiyo ni ile inayosema Hospitali ya KCMC Moshi, imezidiwa wagonjwa na hivyo kupungukiwa mitungi ya gesi. Inasema kwa siku yaani saa 24, mitungi 600 hutumika kwa wagonjwa wa Uviko-19.

Wewe na mgeni mnapigwa butwaa na kujiuliza, hali ikoje huko mitaani kuhusu UVIKO-19. Bila shaka mnahitimisha kwamba hali si shwari, hali ni mbaya kuliko inavyodhaniwa. Watu wanakufa, watu wanapukutika.

Kabla taarifa hiyo kwa ufupi haijamalizika, mwishoni kunakuja taarifa ya Mbio za Mwenge wa Uhuru katika mkoa fulani, inasema Kiongozi wa Mbio hizo kakataa kupokea zahanati! Kisa imejengwa kwa fedha nyingi kuliko bajeti yake.

Inafuatia picha ya umati wa watu waliohudhuria Mbio hizo, wengi hawana cha barakoa wala nini. Bora liende, acha tushangilie Mwenge, kama ni kufa Mungu ndiye anayepanga, aliyetoa ndiye anayetwaa!

Baada ya muhtasari huo wa habari, kinafuata kipindi maalumu ambacho sasa kinawaonesha wanaotambulishwa kuwa wataalamu wa afya, wakitoa elimu kwa wananchi kuhusu kujikinga na UVIKO-19.

Wanasisitiza uvaaji barakoa kwenye mikusanyiko, wanaasa kunawa maji tiririka na sabuni mara kwa mara, na kama hayapo basi vipukusi vihusike, lakini lingine ni kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Mnajiuliza na mgeni wako, hivi hiyo mikusanyiko isiyo ya lazima ni ipi? Kabla hamjapata jibu, linaingia tangazo linasema Jumapili kuna mechi ya kukata na shoka katika uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Anaonekana Mzee Mpili na Mzee Muchacho wakitambiana, lakini pia wanaoneshwa mashabiki wa Simba na Yanga mitaani Kigoma wakipokea timu zao! Wenye barakoa ni wa kuhesabu.

Mnajiuliza tena mikusanyiko isiyo ya lazima ni ipi na ya lazima ni ipi? Majibu pengine ya lazima ni ile ya maziko, kwa maana si rahisi kuacha kuzika, lakini rahisi kuacha kuuguza.

Isiyo ya lazima, mnadhani ni kama hii ya Mbio za Mwenge, Mwenge unaoshikwashikwa na kila mtu bila kujali kanawa au kapukuswa. Kwani msipokimbiza Mwenge nini kitatokea? Mbona JPM alizuia mwaka jana na bado tupo? Isiyo ya lazima; kwani lazima kwenda uwanjani kuangalia mechi ya Simba na Yanga? Kuangalia kwenye luninga kunatosha au? Mbona fainali za UEFA watu hawakwenda uwanjani na bado mechi iliochezwa na mshindi akapatikana?

He, wakati bado mnajiuliza, linaingia tangazo lingine, safari hii mnaambiwa Mbunge wa Morogoro, sijui Kusini au Kaskazini, sijui, Taletale ana tamasha lake la muziki wa kizazi kipya. Daimond atakuwapo.

Vijana wanahanikizwa kuhudhuria tamasha hilo kwa kuwa halitakuwa na kiingilio! Mnajuliza mkusanyiko huu ni wa lazima au si wa lazima? Muziki huo unawapelekea nini wapiga kura wa Taletale kama si UVIKO-19!

Baada ya hilo, ghafla anaonekana mama na mtoto mgongoni, analalamika kwamba amekaa kituo cha mabasi ya mwendokasi muda mrefu mabasi hayaonekani na abiria waliopo ni wengi. Mara basi linafika, hiyo vurumai ya kupanda sasa, acha kabisa!

Watu wanajaa pomoni, wanapumuliana, wanapigiana chafya, wanakoholeana, wanapengeana ni balaa. Barakoa za kuhesabu! Mnajiuliza baada ya hapo ni nini kitafuata? Changamoto ya kupumua ndilo jibu la Watanzania. Tunakufa hatufi? Mungu anajua.

Hivi Watanzania nani katuroga? Hatuoni tena ndoo za maji milangoni! Barakoa zinahesabika! Vipukusi ndiyo kabisaa kwa sababu vinanunuliwa hivyo ni uamuzi tu wa mtu. Nadhani tatizo ni hofu ya kufokewa kama ilivyokuwa, kwamba ukivaa barakoa ulionekana wa ajabu.

Hivi tunashindwa nini kuwa makini kivitendo badala ya kinadharia tunavyofanya sasa? Lazima tukimbize Mwenge? Lazima tujazane kwenye mabasi ya mwendokasi? Lazima tukaangalie mechi za Simba na Yanga na zingine? Hebu tuendelee kujitafakari, vinginevyo Bwana ataendelea kutwaa alichotoa ! **Alamsiki!**

**Wanasisitiza uvaaji barakoa kwenye mikusanyiko, wanaasa kunawa maji tiririka na sabuni mara kwa mara, na kama hayapo basi vipukusi vihusike, lakini lingine ni kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Makato katika miamala ya simu inaakisi maisha ya Watanzania?



Na Thobias Mwanakatwe

KUANZIA Julai 15, mwaka huu, gharama za kutuma na kutoa pesa kwa njia ya simu zilipanda, hivyo kuzua malalamiko nchi nzima.

Malalamiko hayo ya wananchi yamekuja baada ya kuanza kutumika kodi mpya inayoitwa "tozo ya huduma" (service levy).

Kimsingi msimamo wa serikali na nia ya serikali ni mzuri sana kwa kuwa lengo ni kwa ajili ya kukusanya fedha ili kugharamia huduma za maendeleo ya jamii.

Binafsi, sina shaka hilo, lakini huu mzigo wa gharama ulioongezwa unaakisi maisha ya Watanzania wote? Usiangalie familia yako au kipato chako. Tuwaangalie ndugu zetu, jirani zetu, wafanyabiashara wadogo wadogo na watu wengine katika jamii.

Kwa mtazamo wangu naiona hasara kuliko faida. Naiona hasara kwa mawakala, kampuni za simu na watumiaji wa huduma. Kubwa ninaloliona ni kupungua kwa miamala ya kutuma na kutoa pesa.

Mfano ulikuwa, kabla ya mabadiliko hayo, ukitoa kwa Wakala wa Tigo Pesa Sh. 100,000 gharama ya muamala ni Sh. 3,650. Katika hiki kiasi Sh. 3,650 serikali ilikuwa inachukua kodi za aina mbili. Kwanza, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ambayo ni asilimia 18 ya muamala ambayo ni sawa na Sh. 657 kutoka kwenye Sh. 3,650. 'Excise Duty' ambayo ni asilimia 10 ya muamala ambayo ni sawa na Sh. 365 kutoka kwenye Tshs. 3,650.

Kabla ya mabadiliko yalioanza, ukitoa pesa kwa Wakala Tigo Pesa Sh. 100,000 makato ya muamala yalikuwa Sh. 3,650/= katika makato hayo serikali ilikuwa inakuchukua asilimia 28 ambayo ni Sh. 1,022 na kampuni ya simu ilikuwa inachukua asilimia 72 ambayo ni sawa na Tshs. 2,628.

Baada ya mabadiliko, ukitoa kwa Wakala Tigo Pesa Sh. 100,000, gharama ya muamala ni Sh. 3,650 + Sh. 2,530 ya Tozo ya huduma. Kwa maana hiyo kwa sasa ukitoa Sh. 100,000 unalipia Sh. 6180. Kati ya hii Sh. 6,180, kampuni ya simu inachukua Sh. 2,628 sawa na asilimia 43.8 na serikali inachukua Sh. 3,552 ambayo ni sawa asilimia na 56.2.

Kwa haraka haraka unaona Kodi inayotuzwa na serikali ni kubwa mno kuliko mapato ya kampuni. Baada ya kupitia taarifa na makala mbalimbali, nimebaini athari za ongezeko la kodi katika miamala ya simu zinaweza kuwa;-

- Kupungua mzunguko wa biashara za kutuma na kutoa pesa mtandaoni. Ikiwa kuna mtu amenia-hidi Sh. 100,000 kama sina kazi bora nikaifate tu hata akiwa Tegeta. Nitatumia nauli ya Sh. 1,500 au 2,000 kuliko kutumia Sh. 6,180 kwa njia ya wakala.

Na huu ni mfano wa Sh. 100,000 lakini gharama za kutoa kuanzia Sh. 1,000,000 ni zaidi ya Sh. 16,000. Sasa ndugu yangu, yaani nikubali kweli unitumie Sh. 1,000,000 wakati hupo hapa hapa Dar es Salaam, nikiifuata naokoa karibu Sh. 150,000/= nzima. Hapo sijazungumzia ukitaka kutoa Sh. 3,000,000 mpaka 10,000,000 yaani ni maumivu kwa jamii.

- Wateja kupungua katika biashara ya uwakala wa kutuma na kupokea pesa, hivyo hizi ofisi zitaathirika kiuchumi.

- Kampuni za huduma za simu kuna hatihati ya kuyumba kiuchumi kwa sababu wateja wa kutuma na kupokea simu watapungua.

- Ongezeko la kodi linaweza kudumaza maendeleo ya uchumi tofauti na inavyotarajiwa. Idadi ya ofisi za uwakala wa kutuma na kutoa pesa zinaweza kupungua na mitaji ya wafanyabiashara wadogo wadogo itaathirika.

Kwa vigezo hivyo, naiomba serikali iangalie upya hii tozo ya huduma na ikiwezekana ipunguzwe au iondolewe.

Ili kuwa na uhakika wa kipato katika kuendesha nchi jambo kubwa serikali linalotakiwa kufanya sasa ni kutafuta miradi ambayo itaendeshwa na taifa kwa maslahi ya Watanzania wote ambayo itakuwa chanzo cha mapato ya taifa.

Mfano, serikali inaweza kujikita katika kuzalisha umeme kwa wingi na kuuza nchi jirani au serikali kujikita katika uchimbaji wa madini mfano mafuta na gesi kwa manufaa ya wanachi.

Mfano mzuri Libya, Iraq na Syria zilipiga hatua kwa sababu ya mafuta. Zilitumia rasilimali zao ndiyo maana zikaendelea. Urusi nayo moja ya sababu ya maendeleo yake ni uchimbaji wa madini ya chuma.

Nimalizie kwa kusema tozo na kodi ni muhimu katika maendeleo ya taifa lakini nashauri tusitumie muda mwingi kubuni kodi au kufikiria tozo mpya ambazo zitaongeza maumivu kwa jamii.

Pia muda huo wa kufikiria tuutumie kufikiria ni kubuni miradi mikubwa itakayokuwa na tija kwa taifa. Miradi itakayowezesha taifa kupata kipato kikubwa na kugharamia miradi mbalimbali kama wanavyofanya mataifa mengine.

Kwa kufanya hivyo nchi yetu itakuwa na uchumi wa uhakika na uwezo mkubwa wa kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# JE, NI HALALI WAKWE NA NDUGU KUINGILIA NDOA? -2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

**Pia wazazi wengine wamekuwa waamuzi hata pale watoto wao wanapokuwa watu wazima wakiwa na familia zao. Mzazi anaweza hata kumpangia mwanawe ampe fedha kiasi fulani kila mwezi kwa sababu tu yeye ni mzazi.**

WIKI iliyopita tuliangalia kwa kiasi gani baadhi ya mambo yanayosababisha ndugu na wazazi kuingilia ndoa na hatimaye kusababisha wanandoa washindwe kuchukua zipi katika kunusuru ndoa pale tatizo linapojitokeza.

Miongoni mwa hatua hizo husababisha baadhi ya wanandoa huchukua hatua ambazo hatimaye huwadhuru wenyewe, lakini wakati mwingine huyaacha mambo yaende yalivyo. Hii nayo haileti suluhisho kwa kuwa wanaoingilia ndoa hushinda na kuwaacha wanandoa wakiwa na maumivu makubwa.

Miongoni mwa sababu za ndoa kuingiliwa na wakwe au ndugu wa upande mmoja ni pamoja pamoja na familia kutoruhusu watoto kukua. Baadhi ya wazazi hawako tayari kukubali mamlaka yao kwa watoto si ya milele kwa kuwa hufikia mahali ambapo mamlaka hayo yanakuwa na mipaka.

Pia wazazi wengine wamekuwa waamuzi hata pale watoto wao wanapokuwa watu wazima wakiwa na familia zao. Mzazi anaweza hata kumpangia mwanawe ampe fedha kiasi fulani kila mwezi kwa sababu tu yeye ni mzazi. Mzazi anaweza kumpangia mtoto aishi vipi na mkewe au mumewe, awalee vipi watoto wake na masuala mengine ya kimaisha.

Sababu nyingine ni uchumi. Kutokana na umaskini wa familia na kutojikubali kwa wanafamilia hao ambapo hutaka wapewe na mtoto wao kila wanachotaka na wakati wanapotaka, huwa vipofu. Upofu huu huwafanya wasione hali halisi na badala yake kuona hisia zao. Kwa kuwa ndugu yao alikuwa akiwapa mahitaji siku za nyuma na hata kama si kila wakati na kwa kuwa sasa hali hiyo imepungua, ni rahisi kwao kuona kuwa sababu atakuwa mkewe.

Kwa baadhi ya wazazi, watoto wao ni vitega uchumi. Watoto wanapokuwa na uwezo, wazazi hao hutaka kuchuma au kuvuna faida ya kuzaa na kulea. Kutokana na hali hii, mipango ya maendeleo au bajeti ya wanandoa, huweza kutafsiriwa kuwa 'mume kushikwa na mke' au 'mke ni mchoyo' kwa wazazi na baadaye hata kwa ndugu. Kwa kuwa wazazi wanataka kuchuma, lakini kuna bajeti ya familia inayowakwamisha, huanza kumuona mke kama chanzo cha kukwama kwao kuvuna kutoka kwa mtoto wao.

**Sababu zingine ni pamoja na;- Utashi**

Hutokea wakati mwingine mama, dada au hata baba wa mwanamume kutamani, kuomba kushauri au kulazimisha ndugu au mtoto wao amuoe mwanamke fulani. Wanakuwa na sababu zao fulani kutaka jambo hilo lifanyike. Inaweza kuwa ni urafiki tu, kuvutiwa kwao na sura au tabia ya mwanamke anayehusika.

Kwa bahati mbaya muoaji anaweza kupishana nao kiupendeleo au kiutashi, hivyo kukataa ombi, matamanio au amri zao. Bila kujali kama binti mwingine atakayeolewa atakuwa na upendo nao, watamchukia tu. Watamchukia kwa sababu si chagua lao. Watamwona huyu binti kama chanzo cha ndugu au mtoto wao kushindwa kufuata utashi au chaguo lao.

**Vibandiko**

Kama wazazi na ndugu wa mwanamume wana tabia kubwa ya vibandiko (labels) ya humwangalia mtoto au ndugu yao kama ndiye anayewahusu pekee na kumtazama mkewe kama mgeni, tatizo la kuingilia ndoa haliwezi kuepukwa. Haliepukiki kwa sababu hawatataka au kukubali kuona usawa kati ya watu hao.

Mume akitenda haki kwa mkewe kwa mujibu wa sheria na kanuni za ndoa, anaweza kuonekana kuwa ametawaliwa na mkewe, hivyo wazazi au ndugu kuingilia kati. Hawaoni hivyo kwa sababu nyingine bali ni kule kuwawekea vibandiko wanandoa hao mmoja mtu wao na mwingine mgeni.

Suluhisho

Jambo la awali na muhimu kwa wanandoa kulijua ni ule ukweli kwamba, wanapooana hawawi peke yao. Watu wanapooana ina maana kwamba waliofunga ndoa ni hao wawili, lakini kila mmoja kati yao anachukua pia familia mpya. Hivyo, ni kwa vipi ndoa ya watu hawa itakuwa, hutegemea namna kila mmoja atakavyoweza kuishi na familia hiyo mpya au familia hiyo itakavyoweza kumchukulia na kuishi naye.

Tukiwatazama wazazi na ndugu wa wake zetu au waume zetu kama wazazi wetu na kuamini kwamba nao wana nafasi kwa watoto wao, tunajiweka kwenye nafasi nzuri sana ya kumudu kuishi vema na wakwe au ndugu wa mume au mke. Pamoja na kwamba hii peke yake haitoshi kuepusha mikwaruzo kati ya mwanandoa na wakwe au ndugu wa mwenzake, hutuweka katika nafasi ya kuwa wenye haki matatizo yanapoanzishwa na wazazi au ndugu wa wenzetu.

- **Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

Julai 25, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




HUYU NI MSHEHERESHAJI MAARUFU KATIKA SHEREHE ZA HARUSI MBALIMBALI WA MWANZA, MC SARAGATA, AKIONEKANA KATIKA PICHA TOFAUTI AKITENDEA HAKI FURAHA ZA MAHARUSI. ANAPATIKANA KWA NAMBA 0767-544426.

## HARUSI

Ukurasa 12

Ukurasa 15



MAISHA NI NYUMBA

## Fahamu hatua za kutengeneza bustani bora ya maua nyumbani

## Kiazi kitamu chakula na tiba

Ukurasa 14





UREMBO WA NGOZI

## Mwonekano unaopendwa na watu wengi

Ukurasa 14

# Usijilaumu, usimlaumu mtoto jirekebisheni

Na Moses Ismail

Ni hali inayojitokeza kwa wazazi na watoto wengi, na kila inapotokea mzazi na mtoto kila mmoja kwa wakati wake hutafuta sababu ni nini kimewafanya wawe katika hali hiyo.

Kwa vijijini, wazazi wengi hutafuta sababu za chanzo cha kutoelewana na watoto wao kupitia kwa waganga wa kienyeji. Wanachoamini wao ni lazima kutakuwa na mkono wa mtu. Iweje wao na watoto wao wasielewane?

Wanafanya hivyo pale wanapoona watoto wao wakubwa, wenye uwezo wa mali na fedha, wanashindwa kuwasaidia hata kwa mambo yao madogo tu yanayohitaji fedha. Wanaamini hilo haliwezi kutokea bila ya 'mkono wa mtu'.

Hilo limewahi kutokea baina ya Edith Mgaya, mkazi wa Chamazi, nje ya jijini Dar es Salaam. Yeye na mwanae hawakuwa wakielewana kabisa.

Edith anasema: "Ilifikia mahali mwanangu alikuwa hakanyagi nyumbani hata miezi minne mpaka mitano, namuona tu anapita barabarani na gari yake."

Edith akahisi si bure, lazima kuna mkono wa mtu kwa sababu mtoto wake alikuwa na uwezo mkubwa wa mali, akaenda kwa mganga. Anasimulia:

"Kumbe alikuwa amelogwa. Mganga akanipa dawa. Akaniambia nimuite na nijaribu kuongea na mwanangu kwa upole



wakati natumia dawa hiyo. Leo ni mwaka wa sita sasa hatujakwaruzana."

Ni kweli, kwa imani za kiroho uchawi upo na hata vitabu vitakatifu vinaeleza madhara yake na vinakataza waumini kushiriki uchawi, lakini je, katika hili la mzazi na mtoto 'kuwa mbalimbali' ni uchawi ndio unaosababisha?

"Jibu haliwezi kuwa la moja kwa moja", anasema Denis Munga, mtaalamu wa masuala ya saikolojia na kufafanua:


"Haliwezi kuwa la moja kwa moja kwa sababu pamoja na kwamba uchawi upo na watu wanauamini, lakini katika kesi nyingi za mzazi na mtoto kutoelewana suala la saikolojia linachukua nafasi kubwa sana".

Munga anatoa mfano: " wazazi wenye tabia ya kupenda kutokaa pamoja na watoto wao, hawa wanajenga tatizo hilo wenyewe. kutopenda kuwa karibu na mtoto wako wakati akiwa mdogo kunajenga ufa baina yenu.


"Ufa huu ukiendelea kwa muda mrefu, yanakuwa ni maisha ya kawaida baina ya mzazi na mtoto, hata kama mtoto atakuwa na umri wa miaka hamsini, kwa sababu msingi ulishajengwa tangu ututoni".

Wazazi wengi wanaoshindwa kushirikiana na watoto wao katika hali ya utu uzima wanavuna matunda ya ukali waliuonyesha kwa watoto wao walipokuwa wadogo.

Hii inasaidia kwa wazazi wa kizazi hiki kujifunza jambo hilo na kurekebisha pale wazazi wao walipojikwaa kwa malezi yao.




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
AGA, BUA, VAA, AYA, BABU, GOME, VESHWA, VITABU

## AMSHA AKILI





## WATOTO

## PAKA RANGI



## CHEKA KIDOGO



SWALI

Samaki aina ya papa wanapatikana wapi?

MTOTO mmoja alikuwa akicheza na wenzake, mara mvua ilianza kunyesha na wote walianza kushangilia na kuoga. Wakati wakiendelea kuoga maji ya mvua, mama yake alitokea na kuanza kumuonya.

Mama; Kwa nini mnacheza kwenye mvua?

Mtoto: Tulikuwa tunacheza, mara mvua ikanyesha tukajikuta tunaoga?


Mama: Maji ya mvua si mazuri kiafya

Mtoto: Mbona wewe uliniambia mvua sawa na neema?

Mama: sawa, lakini .....

Mtoto: Kama neema na sisi tuache tushangilie.

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mwanamke anapobomoa nyumba yake mwenyewe

KARIBU tena msomaji wangu katika gurudumu la Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo tunamjadili yule mwanamke anayebomoa mji wake, kisha anaanza kutapatapa kumbe kisababishi ni yeye mwenyewe. Au misingi ya asili anakotokea ndiyo inayomtesa.
Wiki iliyopita nilizungumzia kuhusu misingi ya asili yetu na jinsi inavyoweza kutesa wengi katika maisha wanayoishi leo. Ile asili uliyotokea ndiyo inayoratibu maisha unayoishi leo.
Kama hujachunguza misingi ya enzi za mababu, huwezi kujua kwa nini yale unayopitia katika maisha yako yanatokea leo.
Wapo watu walioolewa au kuoa lakini leo ndoa zimebomoka kumbe chimbuko ni asili yao. Tangu zama hizo kwenye familia au koo zao ni watu kuacha au kuachwa tu. Yaani si waolewaji wala waoaji. Wanapata waume au wake wazuri lakini mizizi ya asili yao inakataa.
Maisha yameonyesha hivyo kwa watu walio wengi, lakini hawaelezi sababu. Wale waliokutana na madhila ya aina hii ni muhimu wageuke nyuma wachunguze maisha ya wazazi na hata mababu zao watagundua kuwa roho ya kuoa na kuacha ilishakuwepo kabla. Au roho ya kuachwa na kuolewa kwingine au kuoa wake wengi ilikuwepo vizazi vya nyuma.
Wengine hawatulii kwa waume zao, lazima watafute michepuko hata kama mume ni mtulivu, mchakarikaji, mtunzaji mzuri wa familia. Kinamama wa aina hii ni wale tunawaita viruka njia. Hebu msomaji sikia kituko hiki ujue jinsi shetani anavyovuruga ndoa za wengi kwa mbinu mbalimbali.
Hivi majuzi nilimtembelea ndugu yake kwenye eneo lake la biashara. Tukawa tunazungumzia vituko vya wifi yake anayemnyanyasa mume wake ikiwa ni pamoja na kumpiga kila wakati. Wakati tunaendelea na maongezi akaja mzee mmoja akataka huduma ya maji ya kunywa.
Akapewa maji akaketi. Tukaendelea kuongea huko akisikiliza kwa makini. Ndipo katikati ya mazungumzo mzee akadakiza akasema; "naomba niwakatishe. Vijana wengi leo wanateseka sana kwenye ndoa zao. Kwa mfano nina kijana wangu alifunga ndoa nzuri sana. Mke alionyesha utii na msikivu, mwaminifu. Wakabahatika kuzaa watoto wawili wa kike ambapo mkubwa umri miaka tisa na mdogo miaka minne.
Mume ni mfanyabiashara na pia fundi wa magari. Shida inakuja kwamba kila mume anapojaribu kubuni mradi ili mwanamke aufanye, hataki. Yeye anang'ang'ania kushona nguo. Akaamua kujiunga na vikundi vya ukopeshaji, akakopa fedha lakini mradi wenyewe hauingizi faida kila wakati ni madeni hadi ananyang'anywa vyerehani.
Walikuwa akiishi nyumba ya kupanga kijana akaamua kutafuta kiwanja, akajenga na kuhamia japokuwa haijaisha. Hata hivyo, mwanamke kila siku anatoka asubuhi na kurudi nyumbani usiku kati ya saa nne hadi sita usiku.
Hajali watoto na mara nyingi baba yao akirudi nyumbani huwakuta aidha barazani wanamsubiri mama yao nyumba imefungwa au wanakaa kwa majirani. Na anaporudi mama huwa anawabebea chips na wala hawapikii kwa kuwa ni usiku. Hata awapo nyumbani huwalazimisha kupika na kujifulia nguo. Vituko vyote hivyo huwatishia wasimwambie baba yao.
Mzee huyu akasema ilifikia hatua kijana akamuomba baba yake kiitishwe kikao wanandoa hao waitwe kujua nini kinachoendelea. Katika majadiliano ilibidi mwanamke aombe msamaha wakaendelea na maisha. Hata hivyo, ilimlazimu kijana kuchunguza nyendo za mkewe. Akagundua kwamba yupo mwanamume anayemchelewesha kurudi nyumbani kuhudumia famiia.
Siku moja mama mkewe(mama wa kijana) akafunga safari kwenda kuwaona wajukuu zake akitokea kwenye kongamano la kidini. Majira ya saa moja usiku akafika akakuta wajukuu wapo nje barazani wakamlaki kwa furaha. Milango ya nyumba ilikuwa imefungwa. Kuuliza mama yuwapi wakajibu hajarudi.
Bibi kuona vile ikabidi aulizie kwa mjumbe yakatolewa maelezo na watoto wakasema yote wanayopitia. Mjumbe akaongea na mtendaji ambapo viongozi hao waliridhia bibi aondoke na wajukuu hadi wazazi wao wakapotafutwa kwa melezo.
Mpenzi msomaji, mzee huyo akasema kwamba yule mama aliporudi na kukuta watoto hawapo alipigia simu mama mkwe ili aweze kuongea na wanawe. Hata hivyo watoto walikataa katu kuongea na mama yao.
Msomaji wangu bila shaka umepata picha. Wiki ijayo nitamalizia kilichotokea na kutoa mfano mwingine baba alivyokimbia nyumba kwa kipigo cha mkewe. Je, una maoni? Tuma ujumbe 0715268581.

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Tusifanye mzaha corona ni tishio kwa maisha yetu

WENGI wanaoutafakari ugonjwa wa corona wanaona vifo na watu kuugua kiasi cha kuwa mahututi. Hii ni kwa kuwa inagusa maisha ya binadamu kwa maana ya mwili kuathirika na uhai wa mtu kupotea.

Kwa sasa, waliokufa kwa corona ni zaidi ya milioni tatu duniani na kwa nchini Tanzania, kuna zaidi ya wagonjwa 680 kati yao 27 wamepoteza maisha huku taarifa za serikali zikieleza kuwa hali si nzuri na sasa watu waongeze umakini kwenye kujikinga.

Lakini madhara ya corona nje ya vifo ni makubwa sana hasa kwenye uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla kwa kuwa shughuli za uzalishaji hazitakwenda kwa kasi ile ile kama kipindi hakuna ugonjwa huo.

Pia familia zinatumia gharama kubwa za kutibu wapendwa wao huku kukiwa na malalamiko kuwa bima ya afya haitumiki kugharamia matibabu ya mgonjwa, hivyo na wengi wakilazimika kutumia fedha taslimu.

Aidha, serikali itaelemewa na wagonjwa huku wahudumu wa afya wakiwa ni wale wale na wanakuwa katika hatari zaidi ya kuambukizwa lakini pia nguvu kazi kupotea.

Tangu kuibuka kwa ugonjwa huu, hali ya taharuki imeyakumba maraifa mengi duniani na wapo waliojifungia ndani kabisa kwa zaidi ya siku 14 lakini bado corona iliendelea kuwatesa.

Kwa Tanzania bado wengi hawachukui tahadhari kwa kuvaa barakoa na kunawa mikono. Ni kawaida kwenye vyombo vya usafiri kuona watu wamebanana na wala hakuna anayekumbuka umuhimu wa kujikinga.

Walio kwenye wakati mgumu ambao kama taifa tunapaswa kuwapa moyo na kuwaombea ni watoa huduma kwenye hospitali mbalimbali nchini. Hawa ndio wako mstari wa mbele na hatarini zaidi kupata ugonjwa huu.

Ni muhimu wakatunzwa, wakapewa motisha na kuwa na vifaa vyote muhimu kila wakati wa kazi hizo. Lakini pia ni muhimu kuwapa msaada wa kisaikolojia ili kuwasaidia kwenye afya ya akili kwa kuwa wengi huona wagonjwa mahututi au maiti mara kwa mara. Hakuna kitu kinachoumiza kuona uhai wa binadamu mwenzako unaondoka licha ya jitihada nyingi za kuuokoa.

Athari za corona ni kubwa mno hasa kiuchumi kuanzia ngazi ya familia kwamba sasa kuna mgonjwa au wagonjwa wa kuuguza na fedha zinahitajika na wakati huo huo lazima kuwe na wa kumuuguza maana yake anatakiwa aache kazi na kumuhudumia.

Wako waliopoteza ajira kutokana na athari za corona na wengine wamepata madhara ya kudumu kwenye miili yao hasa mfumo wa kupumua kutokana na ugonjwa huu.

Juzi, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, alizungumza na waandishi wa habari kueleza hali halisi huku akiwashangaa viongozi wa sekta zingine kwa kushindwa kuwajibika ipasavyo katika kuhakikisha wananchi wanachukua tahadhari zote muhimu.

Alipiga marufuku mikusanyiko isiyo ya lazima na kutaka uwajibikaji wa viongozi wa mitaa, kata, wilaya na mikoa katika kuhimiza wananchi kujikinga.

Hadi sasa mikoa iliyoelemewa sana ni Arusha, Mwanza na Kilimanjaro na hospitali za Rufani za KCMC na Bugando zilieleza kuhusu upungufu wa mitungi ya oksijeni.

Cha kushangaza bado wananchi wa mikoa hiyo wanaendelea na maisha kama hakuna ugonjwa, hawachukui tahadhari kama kuvaa barakoa kila wanapokuwa kwenye mikusanyiko.

Kwa ujumla, corona ni janga la kimataifa. Bila kuchukua tahachari kuna uwezekano mkubwa wa kubaki na madhara makubwa kwa kuwa bado chanjo nyingi ziko hatua ya majaribio na hata zilizoidhinishwa bado hazijawekewa dhamana na Shirika la Afya Duniani (WHO) bali madhara yatabaki kwa mtumiaji na kampuni iliyotengeneza chanjo.

Katika kipindi hiki cha wimbi la tatu, lazima kuacha mzaha. Ile imani kuwa hili ni wimbi litapita tu kama likivyopita wimbi la kwanza na la pili, litaangamiza wengi kwa kuwa nguvu ya kirusi ni kubwa hasa maeneo yenye baridi.

Uhai wa mtu ni mali yake mwenyewe ana wajibu wa msingi wa kuutunza. Bila kufanya hivyo ni kuipa mzigo serikali hasa matibabu na kuelemewa kwa huduma za afya.

**Mungu ibariki Tanzania.**



# HUYU NI MSHEHERESHAJI MAARUFU KATIKA SHEREHE ZA HARUSI MBALIMBALI WA MWANZA, MC SARAGATA, AKIONEKANA KATIKA PICHA TOFAUTI AKITENDEA HAKI FURAHA ZA MAHARUSI.





Tunachapicha picha za harusi bure wasiliana kwa namba 0717336368, au barua pepe: Moshilusonzo@Gmail.com" Moshilusonzo@Gmail.com.

# MITINDO

# KAWAIDA SANA LAKINI UNATOKA BOMBA





MWANAUME ni kiumbe kisichojali sana kuhusu uchaguzi wa mavazi, lakini anaweza kuwa na mwonekano mzuri pale atakapoweza kupangilia nguo vizuri.

Hata hivyo, mtu unaweza kuwa na nguo chache, lakini kila siku akaonekana yuko tofauti kutokana na jinsi anavyovaa.

Leo nakupatia mbinu sahihi ya kununua aina ya nguo chache ambazo zitakupa muonekano wa kipekee.

Fulana ya Pamba

Ukitaka fulana itakayo dumu kwa muda mrefu, nunua zilizotengenezwa kwa pamba. Pia, unalazimika kuwa na fulana zenye rangi tofauti, kama nyeupe, nyeusi, rangi ya kijivu, njano, bluu nyepesi na kijani.

Uzuri wa fulana ni kwamba unaweza kuvaliwa na chochote kile.

Fulana za Polo

Mwanamume yoyote anatakiwa kuwa na fulana za Polo zenye kola kwa ajili ya kuzivaa wakati wa mwisho wa wiki.

Mashati ya kawaida

Mashati ya kawaida, ya mikono mirefu au mifupi, ni mazuri kuvaa na jinzi na viatu au raba.

Bukta

Kwa kuzingatia kipindi cha joto kuwa kirefu bukta ni muhimu kuwa nazo.

Kuna aina nyingi za bukta na zenye rangi tofauti. Lakini unatakiwa ziendane na fulana zako na viatu vya kawaida.

Suruali za kawaida

Suruali za aina hii zinaleta furaha kwani zinavaliwa kwenye mazingira mbalimbali. Muhimu kama utakuwa na rangi tofauti.

Jinzi


Jinzi zinaweza kuvaliwa sehemu yoyote ni nzuri kama utakuwa nayo nyumbani.

Ila, ni muhimu kujua saizi yako ile upendeza unavyostahili.

Pia, jinzi zenye ubora zitakuwa na bei zaidi ila bora ununue jinzi yenye ubora itakayodumu kwa miaka kuliko jinzi isiyo na ubora itakyodumu kwa miezi.

UREMBO:
WA NGOZI

# Tango pekee linatosha kukung'arisha



TANGO ni tunda muhimu katika kusaidia afya na urembo wa ngozi kwa mwanamke. Unaweza kula tunda lenyewe, kunywa au kupaka juisi yake na kubandika vipande.

Kulingana na wataalamu wa urembo, njia zote hizo ni nzuri kupata virutubisho muhimu kwa ngozi yako.

Inaelezwa Tango husaidia sana kulainisha ngozi na kuikaza ile iliyopata athari na kulegea.

Pia unapotumia kila mara husaidia kuondoa na kuzuia chunusi makovu, makunyanzi na ukavu wa ngozi ya usoni.

JINSI YA KUFANYA

Chukua tango, maji, chombo cha kuwekea vipande vya tango na kisu cha kukatia vipande vidogo vidogo.

Osha tango lako, chombo chako na kifaa chako cha kukatia tango lako. Bila kumenya, anza kulikatakata tango na ukimaliza kukata chukua vipande hivyo kisha anza kupaka usoni, kuzunguka macho na shingoni.

Acha ikae kwa dakika 15 au 20 na kisha nawa kwa maji safi na uache bila kujikausha. Fanya hivyo kila siku ili kupata matokeo kwa haraka.

Kama unapenda vipodozi vya asili basi tango ni zuri sana kwako. Kula tango, kunywa juisi ya tango, paka vipande na juisi ya matango.

MAPISHI
Na Mary Geofrey

# KIAZI KITAMU CHAKULA NA TIBA

WATU wamekuwa wakihangaika kufanya mazoezi ya kupunguza mwili lakini ipo njia ya kula vyakula vya kusaidia kuupunguza.

**Viazi vitamu na maziwa mtindi**

Viazi vitamu ni vyakula vya wanga ambavyo haviwezi kukunenepesha.

Hii ni kwa sababu ukiachana na wanga kiasi, viazi hivi vina nyuzinyuzi nyingi inayosaidia katika kuchoma mafuta mengi mwilini.

Hivyo hayasababisha uzito kuongezeka kirahisi kama vyanzo vingine vya wanga.

Hivyo ni chakula kizuri sana cha kukupatia nguvu wakati wa diet.

Mtindi una protini nyingi ambayo hufanya mwili ushibe kwa muda mrefu.

Protini pia inachoma nishati nyingi wakati wa umeng'enywaji hivyo inasaidia kuchoma mafuta mengi zaidi mwilini.

Kula viazi vitamu vya kuchemsha na mtindi usio na madoido wowote. Kula asubuhi au mchana kwa kuwa unahitaji nguvu zaidi mwilini wakati huo.

**Matango**

Matango yana maji kwa asilimia 95 hivyo ni tunda zuri kula mara kwa mara bila kuongeza kilo.

Unaweza kuosha vizuri matango yako ukala na maganda yake bila kuchanganya na chochote au kutengeneza kama salad.





# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## FAHAMU HATUA ZA KUTENGENEZA BUSTANI BORA YA MAUA NYUMBANI



ILI nyumba ipendeze zaidi inahitaji kunogeshwa na vitu tofauti ikiwamo bustani nzuri ya maua iliyotengenezwa kwa utaalam.

Nyumba yenye bustani bora huleta utofauti mkubwa na ile ambayo haina kabisa.

Mtaalam wa kutengeneza bustani ya maua eneo la Bunju B, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Mwagi Hassan, anasema utengenezaji wa bustani ya maua hasa katika eneo la nyumbani unahitaji ubunifu na utaalam mkubwa ambao wakati mwingine unatumia akili nyingi.

Anasema ili uwe na bustani bora ya maua, hatua za kuzingatia ni pamoja na kufahamu aina ya maua unayotaka kupanda, kama ni ya kudumu au ni ya muda mfupi.

Pili, anasema baada ya kuamua kuwa bustani yako ni ya aina gani, kinachofuata ni kuamua unayapanda kwa utaratibu upi, kama ni kwa mstari ulionyooka, duara au kwa kufuata sura ya mchoro wa kitu chochote unachotaka, mfano ramani ya Tanzania na nyinginezo.

Hassan anashauri kwamba katika upandaji wa maua, yako yanayomudu juani na ya kivulini, hivyo ni lazima kufahamu mwelekeo wa vitu hivyo ili kutokuathiri ustawi wa bustani yako.

"Kwa mfano maua ya kuzunguka uzio, lazima upande kwa kufuata kipimo kinacholingana hata kama ni kamba, cha muhimu ni kuhakikisha kona moja na nyingine zinalingana ili wakati wa kupanda visipishane na unaweza kupanda maua zaidi ya aina moja ndani ya mstari uliochorwa," anasema Hassan.

Anashauri kwamba kama maua ni mapana, unapaswa kuyapa nafasi ya kutosha ili yapate hewa ya kutosha na nafasi ya kujitanua wakati wa kustawi.

"Na kama udongo wa uzio wako ni mgumu sana au una asili ya mwamba unatakiwa kujaza udongo mwingine kabla ya kuotesha chochote, weka na mbolea kabla ya kuotesha," anasema Hassan.

Anasema baada ya kutengeneza bustani yako na kupandikiza miche ya maua, ni lazima imwagiliwe kila siku kuanzia miche inapokuwa midogo hadi mizizi yake inapochipua na baada ya hapo umwagiliaji wake utategemea na aina ya udongo na hali ya hewa.

# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU ZA NAMNA YA KUCHAGUA REDIO AINA YA SUBWOOFER KWA AJILI YA KUWEKA SEBULENI

1: Hakikisha spika zina mzunguko wa karibu 60-70 Hertz, ili kuchuja sauti na kuwa sikivu.

2: Angalia yenye bei nafuu kulingana na uwezo wako, unaweza kununua ya bei ya juu lakini ikakosa ubora unaotakiwa.

3: Hakikisha vifaa vyake muhimu kama vifungulio, sehemu za kuweka flashi na waya inaonekana vizuri.




KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
'UENYEJI PAMBANO LA WATANI'
MI MWENYEWE SICHEZI KAMALI HATA SIKU MOJA! ILA HAPA TUNABETI LAKI LAKI
KWANI KUNA TOFAUTI GANI ABDALA KUITWA 'DULA?'
SPOTI
UKIPENDA BOGA...
KIGOMA
KUYASUBIRI MATOKEO YA MECHI YA WATANI WA JADI HADHARANI KUNAHITAJI UJASIRI KAMA KULINDA 'MONCHWALI'
NASEMA 'HAMTOKI!'
SHIMONI AU JELA?
KWA JINSI NILIVYOKUWA 'MATINGASI' HATA TUFUNGWE KUMI... SIUMII!
KILABUNI
NAZUNGUSHA ANTENA ANGALIA NDANI
NINI ANTENA! ZUNGUSHA HATA 'UNO' SIENDI NDANI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KAMA UJAUMIA MBONA UNACHECHEMEA?

HABARI KIMATAIFA

# UN yahofia hali ya kiutu Tigray

**Tigray,** ETHIOPIA

UMOJA wa Mataifa (UN), umesema una wasiwasi na hali ya kiutu katika eneo la Tigray Kaskazini mwa Ethiopia, ambako hali ni mbaya kutokana na uhaba wa chakula.

Msemaji wa Shirika la Chakula Duniani (WFP), Tomson Phiri, amewaambia waandishi wa habari kuwa shirika hilo linatoa wito wa kupewa idhini ya kuwafikia watu milioni nne, ambao wanakabiliwa uhaba mkubwa wa chakula na wanahitaji msaada wa dharura.

Phiri alisema WFP imewasilisha msaada wa chakula kwa zaidi ya watu 730,000 katika sehemu za Kusini na Kaskazini Magharibi mwa Tigray katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Idadi hiyo inajumuisha watu 40,000 katika eneo la Zana ambao walifikiwa na msaada wa chakula kwa mara ya kwanza kabisa.

**DW**

# Ulaya yaidhinisha chanjo corona Moderna ya watoto

SHIRIKA la Udhibiti wa Dawa la Ulaya (EMA), limependekeza kuidhinishwa kwa chanjo ya kuzuia maambukizi ya virusi vya corona ya Moderna, kutumika kwa watoto walio na umri wa miaka 12 hadi 17.

Hii ndiyo mara ya kwanza chanjo hiyo kuidhinishwa kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 18.

Katika uamuzi uliotolewa Jana shirika hilo la kudhibiti dawa barani Ulaya lilisema uchunguzi uliofanywa kwa zaidi ya watoto 3,700 kati ya umri huo unaonyesha kwamba chanjo ya Moderna inatoa kinga dhidi ya virusi hivyo.

Chanjo hiyo tayari imeidhinishwa kutumika kwa watu wote wazima kote barani Ulaya.

Hadi sasa chanjo inayotengenezwa na kampuni ya Pfizer na mshirika wake wa Ujerumani BioNTech, ndiyo chanjo ya pekee iliyokuwa imeidhinishwa kutolewa kwa watoto Marekani na Ulaya.

Marekani bado inatafakari iwapo iidhinishe chanjo hiyo kwa watoto.

**DW**

# Mauaji ya watu 13 CAR yazua mkanganyiko

**Kouki,** CAR

KULINGANA na vyanzo mbalimbali, waathiriwa, ambao wanaweza kuwa wengi zaidi, walikuwa vijana, wafanyabiashara, ambao walisafiri kwa pikipiki kwenda katika soko la Kouki.

Serikali mara moja ilishushia lawama muungano wa waasi wa CPC, ambao mkoa huo ni mojawapo ya ngome yake, kuwa ulihusika na mauaji hayo, lakini vyanzo vingi vinashutumu wanajeshi wa Urusi wanaosaidia vikosi vya serikali katika eneo hilo.

Wakati huo huo muungano wa vikundi ya waasi wa CPC ambao uliendesha shambulizi katika mji wa Bangui mapema mwaka ulikanusha kuhusika kwake katika mauaji hayo,kulingana na taarifa ya muungano huo.

Umesikitishwa na kuhusishwa na mauaji hayo bila hata hivyo kusubiri matokeo ya uchunguzi wa kawaida.

Makundi hayo yenye silaha yamebaini kwamba watu waliouawa ni 16 ambao waliuawa na wakufunzi wa Urusi wa kampuni ya jeshi ya Wagner.

Wanamgambo wanaotajwa kama mamluki na wataalam wa Umoja wa Mataifa (UN) ambao pia walitajwa kuhusika na mauaji hayo na kundi la waasi la MKMKS la waziri wa zamani Jean-Serge Bokassa na muungano wa COD-2020 ambao unaleta pamoja viongozi wakuu wa upinzani wa kisiasa.

Wapinzani wanalaani mauaji mabaya na wanadai kuundwa kwa tume huru ya uchunguzi.

Wabunge saba kutoka Mkoa wa Ouham walisema katika barua ya wazi kwamba wamehuzunishwa na mauaji ya raia na wafanyabiashara katika jimbo hilo na kuitaka serikali kutoa mwanga kuhusu tukio hilo.

Tume ya Umoja wa Mataifa, MINSUCA, ambayo imethibitisha kupatikana kwa angalau miili 13, imetangaza kwamba uchunguzi unaendelea na inaomba ushirikiano wa serikali.

**RFI**



Jengo lililoporomoka kutokana na mvua juzi mjini Mumbai, nchini India, juzi. **PICHA: REUTERS**

# Dola milioni 100 kusaidia wakimbizi wa Afghanistan

**Washington,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden ameidhinisha dola milioni 100 katika kushughulikia dharura ya wakimbizi inayohusiana na hali ya nchini Afghanistan.

Katika taarifa yake, Ikulu ya White House imesema fedha hizo zitatoka kwenye mfuko wa dharura na ule wa kusaidia wakimbizi kwa lengo la kukabiliana na dharura ambayo haikutarajiwa ya wakimbizi.

Wakimbizi hao ni wahanga wa mzozo na baadhi ya watu ambao wako hatarini kutokana na hali ilivyo nchini Afghanistan.

Fedha hizo zitawasaidia wale wanaoomba viza maalumu SIVs, ambapo karibu raia 20,000 wa Afghanistan walikuwa wakifanya kazi ya ukalimani na kazi nyingine kuisadia Marekani wakati wa vita na sasa wanahofia kuadhibiwa na Taliban.

Fedha hizo zinaweza kukusanywa kupitia michango ya ufadhili wa mashirika ya kimataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali na yale ya Marekani, iliongeza taarifa hiyo.

Kundi la kwanza la raia na familia zao linatarajiwa kuondolewa nchini Afghanistan kabla ya mwisho wa mwezi huu na watapelekwa katika kambi ya kijeshi ya Fort Lee mjini Virginia wakati wakisubiri mchakato wa viza ukamilike.

Utawala wa Biden unatathmini maeneo mengine ya Marekani na nje ya nchi ambako raia hao wa Afghanistan na familia zao wanaweza kupewa makazi.

Siku ya Alhamis, bunge la wawakilishi la Marekani lilipitisha sheria itakayoongeza idadi ya watu wanaoweza kupatiwa viza maalumu SIVs na kuwapokea karibu watu 8,000.

**DW**

# Mbunge wa upinzani afukuzwa bungeni

**London,** UINGEREZA

MBUNGE wa chama cha upinzani cha Labour Party, Dawn Butler, ambaye alimshtumu Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson kwa kusema uwongo, ameondolewa kwenye kikao cha bunge.

Dawn Butler, katika hotuba yake kwenye Bunge Kuu la Uingereza, alikosoa maneno ya Johnson kuhusu kuvunja uhusiano kati ya janga hilo na ugonjwa mbaya na vifo na akasema kuwa huu ni usemi hatari sana wakati wa janga la corona (Covid -19).

Aligundua kuwa Johnson hakusema ukweli kwa bunge na kwamba alidanganya umma na wabunge mara nyingi, Butler alisema amesikitishwa na hali hii.

Naibu Spika wa Bunge Eleanor Laing, ambaye aliongoza mjadala bungeni, alimwuliza Butler, ambaye alimkatiza, asahihishe taarifa yake juu ya Waziri Mkuu Johnson.

Butler, akihutubia naibu spika, alisema, "Ungependelea nini? Mguu dhaifu au mguu uliokatwa? Unajua, Waziri Mkuu amedanganya bunge mara nyingi.

Inashangaza jinsi yule anayemwambia mwongo, sio mwongo, utata upo hapa.

"Mtu anahitaji kusema ukweli bungeni." Butler, ambaye hakusahihisha madai ya "kusema uwongo" dhidi ya Waziri Mkuu, alifukuzwa kutoka Baraza la huru na naibu spika wa bunge.

**TRT**

MAKALA

# DEMOKRASIA KAMA MSINGI WA MAENDELEO



Na Magabilo Masambu

DEMOKRASIA inayosemwa ni kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi, ambayo viongozi wetu huitumia kuapa wanapoingia madarakani. Ibara ya 8 (1) ya Katiba yetu inasema "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya kidemokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo; (a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii."

"Ni kweli kwamba demokrasia haiwezi kudumu ikiwa wachache hawatakubali matakwa ya wengi. Lakini matakwa ya wengi hujulikana katika majadiliano au mazungumzo ya waziwazi. Kadhalika matakwa ya wachache hujulikana katika majadiliano na mazungumzo.

Bila wale wachache kusema waziwazi matakwa yao, majadiliano hayana maana. Wakati mwingine hata baada ya majadiliano, wachache japo wamekubali kutii uamuzi wa wengi, wanaweza kuendelea kuamini kwamba mawazo yao ni sawa na yaliyo ya wengi yamepotoka.

Demokrasia inawapa haki na ukweli, inawapa wajibu wa kuendeleza mawazo yao mpaka wengi waone kuwa ni ya kweli. Bila hivyo maendeleo katika mawazo hayawezekani" (Tujisahihishe, Uk 3, J.K. Nyerere; 1962)

Lakini msingi mkuu wa demokrasia unaanza na uhuru wa maoni ambao umetamkwa katika ibara ya 18(1) inayosema: "Bila ya kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi."

Watanzania kama taifa, tumekuwa na utamaduni wa kukwepa mazungumzo. Siku hizi hata familia hazikai kama zamani kufanya mazungumzo ya kifamilia. Mama au baba akiwa na jambo anaona haya kulifikisha moja kwa moja badala yake anasubiri mwenza wake aende kwenye shughuli zake kisha anatumia ujumbe wa simu (sms) kufikisha . wengine wanakwenda kuandika kwa mafumbo kwenye mitandao ya kijamii mambo ya familia.

Hii ni hatari kubwa sana kwa taifa. Zamani tulizoea vikao. Palipotokea jambo fulani kwenye familia, watu waliitana kwa ajili ya mazungumzo na ufumbuzi ulipatikana kisha watu kusambaa kila mtu akiwa na ukweli wa jambo.

Demokrasia inaruhusu uvumbuzi au maboresho (innovation). Utamaduni wa kuzuia watu kuzungumza Afrika unatokea kwenye familia. Tumeona mara kadhaa hata shuleni wanafunzi wenye tabia ya kuhoji wakidhibitiwa na baadhi ya walimu wao. Leo watu wengi ambao ni viongozi wetu mahali popote ukiwauliza historia zao watakwambia misukosuko waliopitia na hii ilitokana na uwezo mdogo wa kujibu hoja wa wale waliokuwa wakiwasikiliza.

Watoto katika umri mdogo, wazazi na walimu wao wakiwa na tabia ya kuwakemea na kuwafokea mara nyingi zaidi huwatengenezea udumavu wa fikra. Athari zake wanashindwa kuwa hata wabunifu katika maisha yao maana kila anachojaribu kufanya wanaona watakosea.

Mwisho tunatengeneza taifa la makondoo na mazombi. Matokeo yake wakiwa viongozi watashindwa hata kuhoji juu ya mikataba mibovu dhidi ya rasilimali zetu. Mtu yeyote ambaye hajazoea kuhoji pia ni dhaifu wa kujibu hoja za wengine. Anaona njia nzuri zaidi ni kutumia nguvu kuzima hoja badala ya kuzijibu.

Bahati mbaya tunadhani demokrasia ipo katika usawa wa madaraka pekee. Wanasiasa wengi wanapozungumzia demokrasia hulenga zaidi usawa wa kimamlaka bila kutazama athari nyinginezo zinazotokana na uminyaji wa demokrasia katika nchi. Tujenge utamaduni wa vijana wetu kuwa majasiri wa kujenga hoja zenye ushawishi kuliko kutisha watu. Hawa watakuwa viongozi wa kesho.

Demokrasia ni taa kwa wenye mamlaka. Kama inatumika vizuri, wasio na mamlaka wakisema hapa hamjafanya hivi na vile mnapima kisha yanafanyika marekebisho kesho watakuwa na yapi? Yako ya kupuuza na mengine ni ya kufanyia kazi, unapoyafanyia kazi tayari maendeleo yamefanyika.

Jambo muhimu sana kwa kila kiongozi ni kutofikiri kwamba mamlaka yanampa uwezo wa kiakili zaidi kuliko wengine, hivyo lazima kuyatafakari yale yanayosemwa na wengine na ukitaka kuyafahamu vizuri zaidi ni kukaa nao mezani kama ndugu kujadiliana. Mwisho utagundua kwamba wewe ndiwe uliyekuwa unakosea. Hii ni kwa sababu ukiwa uwanjani ni vigumu kugundua makosa.

Sifa moja kubwa kuliko zingine zote za kuwa kiongozi bora ni kuwa na uwezo wa kusikiliza zaidi hata yale usiyopenda kusikia. Viongozi wengi dhaifu duniani hupenda kusikia yale tu yanayowafurahisha. Utasikiaje mabaya na mazuri? Ni katika uhuru wa maoni na maendeleo yametokana msuguano wa mawazo kwamba hili liko hivi na unaonyesha.

Nguvu hazijawahi kuzaa matokeo mazuri ya muda mrefu bali ni kwa muda mfupi halafu zinaishia pabaya. Tujifunze historia kisha tuchague upande ulio mwema. Viongozi wa Tanzania, lazima wakubali kwamba demokrasia ndiyo kiini cha Ujamaa (Nyerere, J.K 1977 Azimio la Arusha baada ya Miaka 10).

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unakumbuka igizo la Tausi, Siti Binti Kasri?



Na Adam Fungamwango

ILIKUWA hekaheka, patashika nguo kuchanika nchini Tanzania pale muda wa tamthilia ya 'Tausi' ulipokaribia. Kwanza kabisa, siku ya onyesho hilo kwenye televisheni ya ITV, kinamama watapika chakula mapema. Watoto wataoga mapema. Muda ukifika, kinamama na watoto wao kutoka kwenye nyumba hata 10, watakwenda kwenye nyumba ambayo ina televisheni kuangalia mchezo huo.

Nikukumbushe tu hiyo ni mwishoni kabisa mwa miaka ya 90 hadi 2000 mwanzoni. Kama ni kijana wa sasa na hujui ilivyokuwa ni kwamba kipindi hicho si Watanzania wengi waliokuwa na televisheni. Ni nyumba 10 kwa moja. Sehemu nyingine unaweza ukakuta kijiji kizima mwenye TV ni mmoja tu.

Na wale ambao waliokuwa na televisheni kwenye mambo kama ya tamthilia walikuwa hawapendi kuangalia peke yao, hivyo kuwaalika majirani. Hii ipo hata kwenye soka. Ni aghalabu sana mtu kuangalia peke yake.

Hata hivyo kuna baadhi walizitumia kama fimbo ya kuwachapia wenzao kwani kuna wakati walikuwa wanawafukuza, wanawasimanga, ili mradi tu.

Kinamama watakaribishwa kwenye makochi, wengine watatandikiwa mikeka na watoto watakaa chini huku wakipewa maonyo ya kuacha utundu na kutopiga kelele.

Mara utasikika wimbo wa 'Tausi', ulipigwa kwenye miaka ya 1960 na mwanamuziki Mkenya sehemu za Mombasa, Fundi Konde. 'Tausi ndege wangu. Ndege wangu wa fahari. Ndege umekwisha mali, sasa wataka nini? Wapita watu wawili, walioleta ulamali, sasa tuko mbalimbali.'

Wimbo huo ulichukuliwa na ukawa ndio wa kufungulia tamthilia hiyo ambayo ilitokea kuwa maarufu mno nchini na isiyosahaulika kamwe. Yako mambo mbalimbali yaliyoifanya tamthilia hiyo ambayo ilitungwa, kuchezwa na kutolewa nchini Kenya, huku wasanii wote walioigiza wakiwa Wakenya.

Kwanza kabisa, pamoja na kwamba TV ndiyo zilikuwa zinaingia nchini na si watu wengi waliokuwa nazo, lakini televisheni binafsi ndiyo kipindi ambacho zilikuwa zimeanzishwa ikiwamo ITV.

Pili, hakukuwa na filamu na tamthilia za kiswahili wakati huo kwa sababu hakukuwa na televisheni, hivyo ITV kwa kuwapenda waangaliaji wake iliwatafutia tamthilia iliyochezwa kwa lugha ya kiswahili na watu ambao wakati mwingine kuna Mwingiliano wa kitamaduni na ni majirani, yaani Wakenya.

Tatu, huo ndiyo ulikuwa wakati ambao Watanzania walikuwa wanaanza kuangalia televisheni, hivyo bado walikuwa na hamu ya kuangalia vitu mbalimbali. Wengi wanawakumbuka wasanii waliocheza tamthilia hiyo ambao baadhi yao sasa ni marehemu.

Hao ni Maua, Ondieki, Rhoda, Mponda, Shaaban nzao maarufu kama Mzee Kasri, Ashina Kibibi maarufu kama Sitti, Sango, Zinzi, Dk. Kurya, Bibi. Popo, Master Sugu, Sikitu, Jesca Brown, Dama, Rehema na Chokoraa Damu, Kina, Lindi, Vita na Joto.

Yupo pia jamaa mmoja anaitwa Mjuba, halafu kukawa na mganga wa kienyeji aliyeitwa Kalumanzira.

Athari ya tamthilia hii kukawa na watu wakijiita Chokoraa, wakiwa wababe wakaitwa Wajuba, na waganga wa kienyeji wakaanza kuitwa Kalumanzira.

Msanii ambaye tutamzungumzia kidogo hapa ni Ashina Kibibi, ambaye aliigiza kama Siti Binti Kasri. Huyu ndiye mtunzi wa tamthilia hiyo. Ndiyo alikuwa kama staa wa mchezo mzima. Wakati yeye akicheza kama Siti Binti Kasri, akawapa majina yake ya ukweli baadhi ya washiriki, mmoja akawa Ashina na mwingine Kibibi.

Kwa mujibu wake mwenyewe, ni kwamba majina hayo yote ya bibi zake, upande wa baba na upande wa mama. Hakutaka kuweka jina la baba mbele. Alikuja nchini Tanzania mwanzoni mwa miaka ya 2000, bila kujua kama yeye ni staa nchini.

Alifikia eneo la uswahilini Mwananyamala kwa mjomba wake. Pamoja na kuwa ni Mkenya wa Mombasa, Ashina pia alikuwa na asili ya Tanga. Baadhi ya ndugu zake walikuwa Watanzania wa Tanga. Kilichotokea hakuamini. Watu walianza kumfananisha.

Walipoulizia uliziwa na ndugu zake, waliambiwa kuwa ni yeye. Kilichotokea ni kwamba watu walikuwa wanaitana kutoka pande mbalimbali. Nyumba ikazingirwa. Kila mtu si wakubwa si watoto walitaka kumwona Siti Binti Kasri laivu. Wakavunja ukuta wa nyumba.

Magazeti yakaandika ujio wake. Yakatoa picha zake akiwa uwazi japo awali yeye hakutaka hivyo kwa madai ulikuwa ujio binafsi na wa kifamilia. Ndipo walipojigundua kuwa yeye ni staa sana nchini Tanzania na hakupaswa kuja kama alivyokuja.

Utambulisho wake ulimsaidia kupata mikataba ya kufanya maonyesho nchini. Alikuja na kufanya hivyo mara kadhaa. Safari zilizofuata alikuwa akifikia Embassy Hotel na kwenda kwa ndugu zake kusalimia tu na kuondoka na si kukaa huko huko kama mwanzo.

Kwa bahati mbaya sana, Ashina alifariki dunia mwaka 2005 kwa kujinyonga kwenye mti wa mwembe kwao Mombasa.

Tamthilia ya 'Tausi' kwa kiasi kikubwa ndiyo iliyosababisha msukumo wa tasnia ya sanaa ya maigizo nchini. Yalianzishwa makundi mbalimbali likiwamo la Kaole ambalo lilikusanya wasanii mbalimbali wachanga na wakongwe kama vile Mzee Pwagu, Bi Hindu, Fatuma Makongoro aliyejulikana kama Bi Mwenda, Mzee Kipara, Dk. Cheni, Mashaka na Bambo.

Kundi lingine ni la Kidedea ambalo liliundwa na Mohamed Fungafunga maarufu kama mzee Jengua, Makanyanga, Mchikichiki, Peace na wengine wengi ambao wote walibebwa na televisheni ya ITV.

Hapo ndipo baadaye walitoka na kwenda kucheza filamu, maarufu kama bongo movie. Hivyo ukiona filamu za bongo movie, tamthilia mbalimbali za kiswahili nchini, msingi wake haswa ni tamthilia ya 'Tausi' chini ya televisheni ya ITV ambayo imechangia sana kuwapo kwa tasnia hizo nchini Tanzania.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

BAADA ya masaa mwili simu iliita tena, akainyanyua mkono. "Afande nipo kwenye eneo la tukio. Niko wa wenzangu wa kituo kidogo cha polisi cha jirani hapa. Ni kwamba maeneo ya Afrikana tumemkuta mtu amefariki. Ni mwili wa mwanamke ambaye ana miaka kuanzia 23 hadi 26 hivi afande. Ulionekana alfariji kwenye mtaro. Kwa mujibu wa watu hapa wanadhani kwamba huenda ni mmoja wa wanawake makahaba na inawezekana amegongwa na gari, au ameuawa, hilo nadhani litajulikana baadaye uchunguzi utakapofanyika afande."

Ilikuwa ni taarifa fupi ya awali kutoka kwa afande Peter, lakini inayojitosheleza kwa wakati huo.

Inspekta Andrew mpaka wakati huo hakushangazwa na taarifa ya kuokotwa kwa maiti ya mwanamke. Alishaambiwa kuwa kuna zawadi yake na mtu huyo 'muuaji mjivuni'.

Yeye ameshatambua kuwa hayo ni mauaji. Ni kwa sababu ametaarifiwa na mtu aliyeonekana amefurahia kifo hicho. Kitu ambacho ameshangazwa kidogo ni jinsi msichana huyo alipotupwa kwenye mtaro na lengo lionekane kama amegongwa na gari.

Kama isingekuwa sauti ya yule jamaa, inawezekana kila mmoja angejua huenda mwanamke huyo amegongwa na gari.

Ambacho kwa sasa anachosubiri ni taarifa tu ya madaktari ili kazi ianze na kufuatilia ni nani wamehusika kwenye mauaji hayo na pia kumfuatilia mtu ayepiga simu kuitaarifu polisi juu ya mauaji hayo na anahusika vipi.

******************************

"Afande ni kwamba marehemu anaonekana kuwa na majeraha ambayo ni kama alianguka kwenye gari, boda boda au kugongwa na vitu hivyo." Daktari Alfonce alimwambia Inspekta Andrew wakati akimkabidhi ripoti ya uchunguzi wa kifo cha Tausi.

"Ni kwa sababu ana majeraha ya kuburuzika kuanzia kifuani, mbavuni na mguuni upande wa kushoto. Inavyoonekana ni kwamba alipoanguka au kugongwa, aliserereka kwenye barabara, kabla ya kutumbukia kwenye mtaro." Alizidi kuanika ripoti hiyo, huku akiwa pia amemkabidhi nyaraka zilizoandikwa rasmi.




**Ni kwa sababu ametaarifiwa na mtu aliyeonekana amefurahia kifo hicho. Kitu ambacho ameshangazwa kidogo ni jinsi msichana huyo alipotupwa kwenye mtaro na lengo lionekane kama amegongwa na gari.**

"Lakini pia kuna kitu ambacho hadi sasa hivi kina utata na haielewekii imekuwaje."

"Kitu gani daktari?"

"Kichwani tumetoa risasi iliyokuwa imekwama. Hii pia imechangia kwa kiasi kikubwa marehemu kufariki kwa sababu damu nyingi imetoka kichwani. Inawezekana majeraha hayo ya mwanzo yasingemfanya kupoteza maisha. Lakini risasi ya kichwa imechangia sana kifo. Huo niliokwambia ni mukhtasari tu, mengine yote yamo kwenye ripoti."

"Nashukuru daktari kwa sababu kesho nataka kumkabidhi Kamanda wa Polisi wa Kanda ya Kinondoni ili atoe taarifa kwa wananchi ambao wanataka kujua kisa cha binti yule kufariki. Kweli imekuwa ni habari kubwa hapa nchini." Inspekta Andrew alimpa mkono daktari, wakaagana.

Akiwa ofisini, Inspekta Andrew hakutaka kabisa kuihangaisha akili yake kuwa kifo hiki ni cha kawaida.

"Haya ni mauaji." Alijisemea mwenyewe.

Ambacho aligundua ni kwamba muuaji au wauaji hawakufanya kazi yao vizuri. Waliacha shaka kwenye kazi yao.

Kama walimtupa marehemu kutoka kwenye gari, basi wangejitahidi kuhakikisha anakufa. Au wangemmaliza kabisa na kutupa maiti kwenye mtaro. Lakini huenda hawakuwa mahiri kwani wamemtupa mtu ambaye walidhani amekufa, halafu baadaye walivyoona hajafa wakampiga risasi.

Alijua lengo la wauaji ni kwamba ionekane marehemu ni wale wasichana wanaofanya biashara haramu ya ukahaba maeneo ya Sinza na amekufa kutokana na tabia yao ya wizi, hivyo watu wachukulie poa tu.

Sauti ya mtu aliyempigia simu na kutaka kwenda kuchukua zawadi yake pia ilirudia tena kwenye ubongo wake na kuona kabisa kifo cha Tausi kinapaswa kuchunguzwa kwa jicho la tatu na si kijuujuu.

Swali ambalo alitaka majibu yake ni kwamba kweli Tausi alikuwa mmoja wa wale wasichana wafanyabiashara haramu Sinza?

Iwe kweli au siyo ni nani alimuua? Kwa nini? Alipitiwa na usingizi.

****************************

Wiki moja ilipita baada ya mazishi ya Tausi. Donald na Sadiki walikuwa mstari wa mbele kwenye mazishi. Kifupi ni kwamba Donald aligharamia asilimia 90 ya mazishi hayo.

Ingawa alikuwa hajajitambulisha rasmi, lakini tayari baadhi ya ndugu wa Tausi waliufahamu urafiki wao.

Ndiyo maana wala Donald hakupata tabu kukaribishwa na kupewa kipaumbele kwenye mazishi ya mapenzi wake, kitu ambacho kwa kiasi fulani kilimfariji.

Kwa siku tatu, Donald hakurudi nyumbani kwao, wala kwenda ofisini. Alikuwa kwenye mazishi na kulala matanga.

Siku ya nne hakwenda ofisini. Alibaki akijifungia ndani akilia peke yake. Wadogo zake walimfuata na kumuuliza sababu, aliwajibu kuwa anaumwa.

Hata hivyo, baba na mama yake hawakumuuliza kitu chochote. Pamoja na kwamba ilimshangaza kidogo, lakini alipenda sana jambo hilo la kutoulizwa. Hakutaka kuzongwa na maswali ambayo wakati mwingine majibu yake yasingewapendeza. Alichohitaji zaidi wakati huo ni utulivu. Moyo ulikuwa unamuuma kama kaa la moto. Kumkosa Tausi mapema vile ni jambo ambalo hakutegemea kabisa.

Hakujua hatima ya baadaye. Ni kwamba amrejee Doroth au afanye nini. Tausi ameshafariki.

Hili kwanza aliliacha kiporo. Bado alikuwa na mambo mengi yaliyokuwa yanamtatiza akilini.

Aliwaza mengi. Alichokuwa akiwaza ni jinsi kifo cha mpenzi wake kilivyotokea.

Ni jana tu, Kamanda wa Polisi Kanda ya Kinondoni akitoa taarifa ya daktari juu ya kifo cha msichana huyo ambapo ilisemekana pamoja na kudaiwa kurushwa kutoka kwenye bodaboda au gari, lakini pia iligundulika kuwa alipigwa risasi kichwani.

"Ina maana Tausi aliuawa. Nani alimuua?" Alijiuliza. Baadaye alikumbuka maongezi yake na Sadiki, kabla ya kwenda Magomeni Makuti baada ya kutoonekana kwa siku tatu.

**INAENDELEA JUMAPILI**

# SHATTI ASAMBAZA BONGO FLEVA KUTOKA JAPAN




TANZANIA imebarikiwa kuwa na vijana wengi wenye vipaji lukuki ambavyo kama vikitunzwa na kupewa nafasi vinaweza kuishangaza Dunia.

Miongoni mwa vijana hao ni Shatti, msanii wa muziki wa kizazi kipya ambaye kwa sasa anaishi Japan huku akiendelea na sanaa yake chini ya usimamizi wa lebo ya Cutsleeve Records yenye asili ya Jamaica.

Jina lake kamili ni Rashid Sameer Mrisho, ambaye alizaliwa Februari 12, mwaka 1999 jijini Dar es Salaam kwa wazazi Rashid Mrisho na Siaminah Kombakono.

ALIVYOANZA SANAA YA MUZIKI

Shatti, anasema alianza kupenda muziki akiwa mdogo kwa kusikiliza kazi za wasanii nguli duniani, hivyo akajenga uwezo wake binafsi wa kufanya aina mbalimbali za muziki kama Dancehall na rap.

"Nilikuwa nasikiliza wasanii wakubwa kama Bob Marley, Peter Tosh, Michael Jackson, Tupac, Biggie na wengine ambao walinisaidia kukuza kipaji na uwezo wangu wa kufanya muziki," amesema Shatti.

Uwezo wake unampa makali kama msanii ili ateme muziki mzuri ambao unafanya aorodheshwe kama Mfalme Mpya asiye na ubishi wa Dancehall, mwimbaji na mtunzi mahiri wa nyimbo.

MAISHA YAKE JAPAN

Shatti aliondoka Tanzania kwenda Japan baada ya kumaliza elimu ya sekondari katika Shule ya Sekondari ya Benjamin Mkapa iliyopo Dar Es Salaam.

Msanii huyu sasa anajulikana kwa maelfu ya marafiki, familia ya muziki na mashabiki kama Shatti ambapo mwaka jana alipata umaarufu kama msanii anayekua haraka.

AACHIA 'BLAZIN HOT'

Meneja wa msanii huyo HIRO anasema unaweza kuendelea kumpa sapoti Shatti katika safari yake hii ya muziki ili azidi kufanya vizuri kwenye Dancehall, rap na Hip hop.

"Tumeachia ngoma mpya inaitwa 'Blazin Hot', hivyo nahitaji mashabiki kuupokea ili azidi kufanya vizuri." Amesema.

Kupitia mitandao ya kijamii anapatikana katika Instagram kwa majina ya @Shatti_tz, @jdartmuzik na @cutsleeve_records.

## HABARI MICHEZO




# ALABA
## SIWEZI KUWA KAMA RAMOS

**MADRID, Hispania**

DAVID Alaba amesema kwamba, hawezi kuwa beki mkamilifu zaidi ya aliyekuwa nahodha wa Real Madrid, Sergio Ramos hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Alaba ambaye ni raia wa Austria, alisajiliwa rasmi Real Madrid Mei, 2021 baada ya mkataba wake kule Bayern Munich ya Ujerumani kumalizika.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 sasa amepokea jezi namba nne mgongoni iliyokuwa ikivaliwa na Ramos hapo Madrid.

Ramos aliyehudumu Real kwa kipindi cha miaka 16, alijiunga na Paris Saint-Germain akiwa mchezaji huru.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 35 alisaini mkataba wa miaka miwili pale PSG ambayo inanolewa na kocha zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino.

"Ramos alikuwa hapa kwa muda mrefu na alivalia jezi namba nne mgongoni. Nitajituma ila huenda nisiwe kama yeye," alisema Alaba akiwaambia wandishi wa habari.

Ramos ambaye anajivunia rekodi ya kuichezea Hispania mechi nyingi zaidi za kimataifa, alishinda mataji manne ya LaLiga akiwa na Real Madrid, na manne ya Ligi ya mabingwa Ulaya.



# POCHETTINO AJIFUNGA PSG HADI 2023

**PARIS, Ufaransa**

PARIS Saint-Germain imetangaza kwamba, kocha wake mkuu, Mauricio Pochettino amesaini mkataba utakaomuweka klabuni hapo hadi mwaka 2023.

Pochettino aliwasili kwa miamba hao wa Ligue 1 mwanzoni mwa Januari mwaka huu, akichukua nafasi ya Thomas Tuchel, ambaye kwa sasa ni kocha mkuu wa Chelsea.

Mlinzi huyo wa zamani wa PSG msimu uliopita alizidiwa nguvu na Lille waliotwaa taji la Ligi Kuu ya Ufaransa.

Walishinda taji la Coupe de France, pamoja na kufika nusu fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya.

Awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Tottenham, ambako alifukuzwa Novemba 2019, lakini sasa Pochettino amekubali kuongeza mkataba wa miaka miwili kubakia hapo Paris.

"Nina furaha kubwa hapa, kwa upande wangu na benchi zima la ufundi," alisema Pochettino akinukuliwa na tovuri ya PSG.

" Ni muhimu sana kwa upande wetu kuhisi kujiamini kwa klabu na kunatupa sisi uwezo mkubwa wa kufikia malengo yetu."

# ABRAHAM ANUKIA ARSENAL

**LONDON, England**

ARSENAL inakaribia kuipata saini ya mshambuliaji wa Chelsea na England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, kwa mujibu wa Sky Sport.

Abraham msimu uliopita hakuwa na nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea na sasa amewekwa kwenye orodha ya kuuzwa.

Nyota huyo pia ni mmoja ya wachezaji wanaowindwa sana na Tottenham Hotspur na Inter Milan, kwani Chelsea imeonekana kuwa haina mpango wa kuendelea kuwa naye kwa msimu ujao.

Chelsea inataka kumuuza Abraham ili kupata kiasi cha fedha inachoweza kukitumia kumsajili straika mmoja kati ya Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, Romelu Lukaku mwenye miaka 28, au Erling Haaland katika dirisha hili.

Nyota huyo sio mchezaji anayeonekana kuwa kwenye mipango ya kocha Thomas Tuchel kwa msimu ujao kwani hata katika michezo ya mwisho msimu ya uliopita alikuwa hapewi nafasi ya kutosha kwenye kikosi cha kwanza.

Na kwa mujibu wa ripoti, Arsenal ndio ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kupata saini ya mchezaji huyo katika kipindi hiki cha majira ya joto.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANCHESTER CITY MGUU SAWA KWA GREALISH

Maslahi binafsi yafikiwa na sasa wajiandaa kutoa pauni mil. 90...

**MANCHESTER,** England

WINGA wa England, Jack Grealish amefikia makubaliano binafsi na Manchester City, kwa mujibu wa Football Insider.

Mashabiki wa England walikuwa na hamu kubwa ya kumshuhudia Grealish kwenye michuano ya Euro 2020 na alikuwa na kiwango cha kuvutia.

Nahodha huyo wa Aston Villa alikuwa akimulikwa na klabu kadhaa kubwa za Ligi Kuu England, huku klabu yake hiyo ikionesha nia ya kutotaka kumuachia aondoke kipindi kilichopita cha usajili na kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto.

Mapema Januari mwaka huu, Manchester United walikuwa kwenye nafasi nzuri ya kumsajili Grealish, kabla ya dili hilo kushindikana.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, Grealish anakaribia kuondoka Aston Villa na kutua kwa mabingwa wa Ligi Kuu England, Man City.

Taarifa zaidi zinasema kuwa, tayari Grealish na Man City wamefikia makubaliano binafsi na sasa kilichobaki ni mazungumzo ya klabu hizo mbili.

Kwa hali jinsi ilivyo, Aston Vila hawana uwezo wa kumbakiza Grealish katika kikosi hicho kipindi hiki cha majira joto, na ni wazi kwamba, msimu unaokuja hatakuwa tena katika viunga vya pale Villa Park.

Licha ya kukulia na kuwa shabiki wa Villa na kutumia muda wake mkubwa kucheza katika klabu hiyo, pia alicheza kwa muda mfupi kwa mkopo kule Notts County.

Na sasa ni wazi kwamba, hata Grealish mwenyewe anataka kujaribu changamoto mpya katika klabu kubwa ili pia aweze kuingia kiasi kikubwa cha fedha.

Ripoti hiyo imebainisha kwamba, Man City ipo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 90 ili kumsajili Grealish na ni wazi kwamba, itakuwa ngumu kwa Villa kukataa kiasi hicho cha fedha.

## KWA UFUPI

### CHELSEA WAKOMAA NA HAALAND

CHELSEA inatarajiwa kutoa dau la pauni milioni 130 kumnunua mshambuliaji wa Borussia, Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri w amiaka 22, baada ya mmiliki wake Roman Abrahamovich kutoa baraka zake kuendelea na kile ambacho kitakuwa rekodi mpya ya klabu hiyo. (Football Insider)

### DAU LA HAALAND

INTER Milan inataka dau lisilo chini ya pauni milioni 102.5 kutoka Chelsea ili kumuuza mshambuliaji wa Ubeligiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28. (Metro)

### GREALISH HUYO CITY

MANCHESTER City wamefikia makubaliano na kiungo, Jack Grealish na wako tayari kuipatia ofa ya pauni milioni 90 kwa Aston Villa ili kumsajili mchezaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 25. (Football Insider)

### KANE BADO CITY

MANCHESTER City imesema kwamba, ripoti zinazosema klabu hiyo imeafikiana na Tottenham kumsaini mshambuliaji wa England, Harry Kane kwa dau la pauni milioni 160 ni upuzi (Manchester Evening News)

### HARRY HAUZWI

TOTTENHAM Hotspur imesisitiza kwamba, haina mpango wa kumuuza nahodha wake, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 kipindi hiki cha majira ya joto. (Football London)

### UNITED YASUBIRI KWA POGBA

MANCHESTER United inasubiri ombi kutoka kwa PSG msimu huu la kumtaka kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28. (Telegraph)

### MBAPPE AKATAA

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, ameiambia PSG kwamba, hatoongeza mkataba wake ambao unakamilika mwaka 2022. (AS)

### CAMAVINGA BADO

KIUNGO wa kati wa Rennes na Ufaransa, Eduardo Camavinga anataka kuhamia Hispania baada ya mazungumzo kati ya Manchester United na wawakilishi wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kushindikana. (Manchester Evening News)

### GRIEZMANN NA JUVE

BARCELONA inaamini kwamba, iwapo mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo ataondoka Juventus msimu huu, klabu hiyo ya Italia itakuwa tayari kumnunua kwa mkopo mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30. (Sport)

### LACAZETTE KUUZWA

ARSENAL haitamuongezea mkataba mshambuliaji wa Ufaransa, Alexandre Lacazette na imetoa ofa ya dau la pauni milioni 15 kwa mchezaji huyo ili kusaidia timu hiyo kupata fedha za kumnunua mshambuliaji wa Chelsea mwenye umri wa miaka 23, Tammy Abraham. (Sun)

### NEWCASTLE YAKOMAA NA WILLOCK

KOCHA wa Newcastle United, Steve Bruce amesisitiza kuhusu mpango wa klabu hiyo kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal mwenye umri wa miaka 21, Joe Willock. (Sky Sports)

# COASTAL UNION, MBOSSO WAMLILIA WAZIRI ALLY

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imeeleza kupokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha mwanamuziki maarufu nchini, Waziri Ally (pichani) ambaye ni shabiki mkubwa wa timu yao, kilichotokea usiku wa kuamkia jana kwenye Hospitali ya Mwananyamala, Dar es Salaam.

Wakati huo msanii Mbosso andika kwenye mtandao wake kuwa msanii huyo amefariki wakiwa wanatarajia kutoa ngoma iitwayo 'Tulizana' ambayo walikuwa wameshamaliza kupiga picha za video.



Kwenye mtadao rasmi wa klabu hiyo, Coastal imetoa picha ya marehemu Waziri, akiwa amevaa jezi ya timu hiyo na kuandika.

"Klabu ya Coastal Union tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha shabiki wetu mkubwa na mwanamuziki nguli nchini Wazir Ally aliyefariki jana (juzi). Kwa niaba ya uongozi, wanachama, wapenzi na mashabiki wa Coastal Union tunatoa pole kwa ndugu jamaa na marafiki kwa kuondokewa na mpendwa wao." Iliandikwa taarifa hiyo.

Msanii wa bongo fleva, Mbosso pia alionyeshwa kuguswa na kifo hicho na kuandika kwenye mtandao wake wa kijamii maneno yafuatayo.

"Dah. mzee wangu Waziri Njenje. Tulifanya wimbo wetu salama. Tukasafiri mpaka Tanga. 'tukashuti' video yetu salama kabisa na hivi juzi tu hapa tumeongea kwa furaha kabisa tukiwa tunapanga kutoa video ya wimbo wetu 'Tulizana'. Leo umeenda baba, dah. Mungu akupe kauli thabiti mzee wangu." Aliandika.

Kwa mujibu msemaji wa familia, Aboubakar Liongo, marehemu alifariki kwa ugonjwa wa moyo ambao alikuwa nao, lakini alikuwa akipata matibabu huku akiendelea na shughuli zake.

Waziri alianza kupata umaarufu akiwa mwishoni mwa miaka ya 1970, akiwa na Juwata Jazz, wana Msondo Ngoma na kupiga kinanda mwenye nyimbo mbalimbali, ikiwemo iliyompatia umaarufu 'Sogea Karibu', ambao alikipapasa kwa umahiri mkubwa.

Aliihama Msondo na kuasisi kundi la Kilimanjaro Band wana Njenje mwanzoni mwa miaka ya 1980, na kutoa nyimbo nyingi kama 'Njenje,' 'Kachiri', 'Kinyaunyau', 'Gere', 'Ndembele', 'Boko', 'Tupendane', na nyingine nyingi.

Marehemu anatarajia kuzikwa leo kijijini kwake Pongwe, mkoani Tanga.




Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Kigoma (KFA), Omar Gindi (kulia), akizungumzia maandalizi ya mchezo wa fainali ya Kombe la FA utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika kati ya Simba na Yanga zote kutoka jijini Dar es Salaam. **PICHA: SOMOE NG'ITU**.

# Ligi ilikuwa na mvuto - Kichuya

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa Namungo FC, Shiza Kichuya amesema kuwa Ligi Kuu msimu huu, ilikuwa nzuri, bora, yenye msisimko na mvuto wa aina yake.

Akizungumza Dar es Salaam, Kichuya pia ameipongeza timu yake ya zamani ya Simba kutwaa ubingwa na kusema ilistahili kwa sababu ilijipanga vema ndani na nje ya uwanja kwa maana kuwa na wachezaji bora, maandalizi pamoja na uwezeshwaji.

"Msimu huu bwana ligi ilikuwa ngumu, nzuri, ilikuwa na ushindani na mvuto mkubwa. Ni moja kati ya ligi bora nilizowahi kucheza. Japo imechelewa kumalizika, lakini ilikuwa na msisimko sana. Tumeona kabisa kwenye ligi hii, timu ambayo huwezi kuitarajia inakwenda kupata matokeo kwenye timu nyingine ambayo haikudhaniwa," alisema Kichuya.

Kuhusu majaliwa yake kwenye soka, Kichuya alisema kuwa mashabiki watarajie kumuona kwenye klabu yoyote, akiwa ametinga jezi ya aina yoyote kwa sababu yeye kazi yake ni kucheza mpira.

"Mimi kazi yangu ni kucheza soka. Na nashukuru nilikuwa na mambo fulani hivi yalikuwa hayajakaa sawa, lakini kwa sasa kila kitu kinakwenda vizuri, hata mimi mwenyewe najiona kuwa niko vizuri. Kiwango changu kimeanza kurudi, kwa hiyo mashabiki watamuona yule Kichuya waliomzoea msimu ujao," alisema.

Kichuya ambaye baada ya mechi kati ya timu yake ya Namungo dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikatundikwa mabao 4-0, alibadilishana jezi ya Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema mchezaji huyo ni rafiki yake tangu wakiwa wadogo kwenye michuano ya Coca Cola, hivyo hiyo ni kawaida yao kila wanapokutana, hasa wakiwa kwenye timu tofauti.

## Biashara yaja na majembe mapya CAF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Biashara United imesema kuelekea kwenye michuano ya kimataifa itasajili wachezaji wengine kwenye maeneo ya ushambuliaji, ulinzi na kiungo ili kuboresha kikosi hicho kwa ajili ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Haji Mtete, amesema kuwa wamepokea ripoti ya mwalimu Patrick Okumu na hata kabla hawajakaa kikao na kuipitia, lakini dodoso la awali lilionekana kabisa kuwa anahitaji wachezaji maeneo ya ushambuliaji, ulinzi na kiungo.

"Tunakwenda kucheza mechi za kimataifa. Tunakwenda kucheza michuano mikubwa na wachezaji wa viwango vya juu kwa hiyo na sisi lazima tujiimarishe. Lengo letu ni kwenda kwenye michuano hiyo tukiwa na wachezaji wenye viwango vikubwa na wazoefu. Tayari tumepata uzoefu kutoka kwenye Ligi Kuu ya Tanzania, lakini pia tumejifunza kutoka kwenye timu ambazo zimeshiriki michuano ya kimataifa na kujua nini kinahitajika," alisema Mtete na kuongeza.

"Katika dodoso lake, kocha wetu walisema kuwa anataka washambuliaji, mabeki na viungo wa kati. Tunakwenda kukaa chini sasa na kupitia ripoti yake rasmi, baada ya hapo tufanye anachokihitaji kwa ajili ya kuingia uwanjani," alisema.

Alipoulizwa kama wachezaji hao ni kutoka nje au Tanzania, Katibu Mkuu huyo alisema kuwa itakuwa mchanganyiko, na kama watu hawajui ni kwamba wao pia wana uwezo wa kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi na kwa uthibitisho ni kwamba wanao wachezaji kutoka Ghana, Kenya na Uganda ambao wamecheza Ligi Kuu msimu huu, hivyo haitokuwa ajabu wakashusha majembe kutoka nje ya nchi.

## Kigoma waelekeza nguvu Ligi Kuu Tanzania Bara

**Na Somoe Ng'itu, KIGOMA**

CHAMA cha Soka Mkoa wa Kigoma (KFA), kimesema Ligi Ngazi ya mkoa nimepangiwa kufanyika katika viwanja mbalimbali kuanzia Julai 28, mwaka huu.

Katibu Mkuu wa KFA, Omar Gindi aliliambia gazeti hili maandalizi ya ligi hiyo yamekamilika na jumla ya timu 18 zimethibitishwa kushiriki michuano hiyo.

Gindi alisema ligi hiyo itachezwa kwa mtindo wa nyumbani na ugenini huku akizikumbusha timu zote kufuata kanuni na taratibu za mashindano hayo ya juu katika ngazi ya mkoa.

Kiongozi huyo alisema wanaamini bingwa atakayepatikana atakwenda kuiwakilisha vyema Kigoma kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa wa mikoa (RCL), mwakani na hatimaye kupata timu itakayopanda daraja.

" Malengo yetu ni kupata timu ya kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, kupitia hamasa ya fainali ya Kombe la FA, tunataka kuendelea kuwaletea burudani mashabiki wa Kigoma, tunaitazama na tuseme ukweli tuna kiu ya kucheza Ligi Kuu," alisema Gindi.

Michezo
Jumapili Julai 25, 2021
Nipashe



Man City mguu sawa kwa Grealish

HABARI UK 22

## Coastal, Mtibwa zabaki Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Coastal Union na Mtibwa Sugar, zimefanikiwa kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupata matokeo mazuri kwenye mechi zao mbili za mchujo dhidi ya Pamba na Transit Camp ambazo zimetoka Ligi daraja la Kwanza.

Jana kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Coastal Union ilichapa Pamba kutoka Mwanza mabao 3-1 na kuifanya timu hiyo kushinda jumla ya mabao 5-2, kwani Jumatano iliyopita timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza.

Mtibwa nayo imefanikiwa kubaki Ligi Kuu, licha ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Transit Camp kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro, kwani kwenye mechi ya kwanza kwenye Uwanja wa Uhuru, Jumatano iliyopita, Mtibwa ilishinda mabao 4-1.

Kwa maana hiyo Mtibwa imebaki Ligi Kuu kwa jumla ya mabao 4-2.

Licha ya kuokoa mkwaju wa penalti dakika ya 43, kipa wa Pamba, Samuel Simon, alijifunga bao dakika moja kabla ya mechi kumalizika na kuipatia Coastal Union bao la tatu.

Winga machachari wa Coastal Union Abdallah Selemani 'Sopu', aliipatia timu yake bao la kwanza kwa mkwaju wa penalti dakika ya 30, lakini alikosa penalti nyingine dakika ya 43.

Sopu pia alifunga bao la pili mkwaju wa faulo, kabla ya kipa wa Pamba kujifunga mwenyewe bao la tatu.

Kwenye mechi hiyo ya 'play off', Pamba ilianza kupata bao mapema tu kwenye dakika ya 10, baada ya beki wa Coastal Union Peter Mwangosi kujifunga mwenyewe akiwa kwenye harakati ya kuokoa.

Mchezaji aliyeipatia Transit Camp bao la kufutia machozi kwenye mechi ya Jumatano, Karegea Hazanga dakika ya 56, ndiye aliyefunga bao pekee kwa timu hiyo, ikishinda bao 1-0, lakini akishindwa kuifanya timu yake hiyo ya maafande wa JWTZ kusonga mbele.



Mshambuliaji wa Simba, Chris Mugalu (mwenye mpira), akimiliki mpira mbele ya beki, Joash Onyango na Miraji Athumani (kulia), katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma jana asubuhi. **PICHA: SOMOE NG'ITU.**

# SIKU YA HUKUMU IMEWADIA

## ●●● Simba yasema haina presha wakati Yanga ikisisitiza lazima mwali atatua...

**Na Somoe Ng'itu, KIGOMA**

HATIMAYE siku iliyokuwa inasubiriwa na mashabiki wa soka ndani na nje ya Tanzania imefika kwa watani wa jadi Simba na Yanga kukutana katika mchezo wa fainali ya Kombe la FA utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani hapa.

Vigogo hao wanakutana ikiwa ni siku 22 zimepita tangu walipocheza mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo Yanga aliibuka na ushindi wa bao 1-0, na kumchelewesha mtani wake kutangaza mapema ubingwa wake wa msimu uliomalizika.

Lakini Yanga itaingia uwanjani tena ikiwa na kumbukumbu ya kuifunga Simba katika fainali za Kombe la Mapinduzi mapema mwaka huu huku ikilazimishwa sare ya bao 1-1 kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema amekuja mkoani hapa wa kazi moja ya kuchukua kikombe hicho kilichobakia katika msimu huu baada ya kuchukua kwa mara ya nne mfululizo ubingwa wa Bara.

Gomes alisema hana wasiwasi wowote kuelekea mchezo huo na amejiandaa kuingia kivingine katika fainali hiyo inayochezwa kwa mara ya sita tangu kuanzishwa kwa mashindano hayo.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wote wako Kigoma na hana majeruhi hivyo leo atakuwa na wigo mpana wa kupanga kikosi kitakachoanza.

"Sina presha yoyote katika mchezo huu, tunahitaji ushindi tu, nimeshaiangalia Yanga kuanzia katika maeneo ambayo wako imara na yenye upungufu, katika ligi ambao walikuwa ni wapinzani wetu, tuliwazidi pointi tisa, haikuwa kazi rahisi," alisema Gomes.

Aliongeza naye ameshayafanyia kazi upungufu yake na anahitaji kumaliza mechi mapema ili kuwapa heshima mashabiki wao ambao ndio muhimu zaidi.

"Tumejiandaa vizuri, Uwanja kwetu si tatizo, tuko tayari kucheza katika mazingira yoyote, ninajivunia wachezaji wangu na wako imara katika hilo, wanaonyesha ushirikiano mkubwa, tumejipanga kumaliza vizuri msimu na si kulipia kisasi," Gomes aliongeza.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' alisema wachezaji wote wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo wa wameahidi hawatawaangusha mashabiki wao.

"Tunamshukuru Mungu tuko salama, hatuna presha ya aina yoyote, presha iko kwa mashabiki, tunawaahidi tutaingia kupambana na hatimaye kunyanyua Kombe," alisema Zimbwe Jr.

Naye Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh alisema timu yao iko katika hali nzuri na kila mchezaji anatarajia kujituma na kucheza katika kiwango bora ili kufikia malengo.

Hafidh alisema katika mchezo huo Yanga itakosa huduma ya Abdallah Shaibu 'Ninja' ambaye ni majeruhi na Haruna Niyonzima ambaye ni mgonjwa.

"Tuko imara na tunatarajia kukamilisha vizuri jambo letu, tutacheza kwa tahadhari kwa sababu mechi hii inahitaji umakini na utulivu zaidi," Hafidh alisema.

Omar Gindi, Katibu Mkuu wa Chama cha Soka cha Mkoa wa Kigoma (KFA), aliliambia gazeti hili maandalizi ya mchezo huyo hadi kufikia jana mchana yalikamilika kwa asilimia 95 na amewataka wageni wote waliofika mkoani hapa kuwa na amani.

Gindi alisema wameandaa utaratibu mzuri wa kuingia uwanjani kwa kutumia mageti nane na yatafunguliwa kuanzia saa 3:00 asubuhi huku barakoa zikitolewa bure kwa wote watakaoingia uwanjani.

Alisema hadi kufikia jana mchana, jumla ya tiketi 12,000 zilishauzwa huku Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), likiwashukuru wamiliki wa uwanja kwa ushirikiano walioonyesha kuanzia katika hatua za awali za maandalizi ya mchezo huo.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042